Nipashe
Jumamosi Agosti 1, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580299
The Guardian digital
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




UKURASA 11



## Chanzo cha ajali boti iliyoua 10 Ziwa Tanganyika chatajwa

UKURASA 3

# Majaliwa akemea kauli za uchochezi

UKURASA 2



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akijadiliana jambo na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambaye pia ni Mgombea Urais wa Zanzibar Mteule wa CCM, Dk. Hussein Ali Mwinyi, baada ya Baraza la Eid El Hajj katika ukumbi wa Bumbwini, Kaskazini B, mkoa wa Kaskazini Unguja jana. Dk. Shein, alitumia baraza hilo, kuaga rasmi wananchi wa Zanzibar. **Picha zaidi Uk. 7. PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## MASHEHE WAONYA VURUGU UCHAGUZI

UKURASA 3

## Ziara za JPM zinavyoacha maumivu kwa wateule wake

UKURASA 2

Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store



**MICHEZO** TSHISHIMBI AMWAGA MBOGA RASMI YANGA UK.24

**MAONI, KATUNI UK.6**

# Ziara za Magufuli zilivyoacha maumivu

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli ametengua uteuzi wa Mkuu wa Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani, Juma Njwayo, ikiwa ni muda mfupi baada ya msafara wake kusimama wilayani humo na kubaini dosari katika utendaji wa wateule wake.

Juzi, Rais Magufuli alibaini dosari hizo alipokuwa njiani kwenda Dar es Salaam akitokea Lupaso, Masasi mkoani Mtwara alikokwenda kuongoza maziko ya Rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa.

Baada ya msafara wake kusimama wilayani huko, alishtushwa na taarifa za mkuu huyo wa wilaya kutokuwa na gari, pia gari la kaimu mkurugenzi mtendaji wa halmashauri lina matatizo na magari ya kubebea wagonjwa wilayani huko ni mabovu, hivyo kuagiza uchunguzi ufanyike.

Baada ya maelezo hayo, Rais Magufuli aliahidi kuyafanyia kazi na kuwatuma mawaziri wa sekta husika kwenda kuyashughulikia.

Muda mfupi baadaye, Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa, alitoa taarifa ikijulisha kwamba, Rais Magufuli amemteua Luteni Kanali, Patrick Sawala, kuwa Mkuu wa Wilaya hiyo na ametengua uteuzi wa Njwayo.

Matukio yanayofanana na hilo ni pamoja na lile la Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Wilson Kabwe (marehemu) ambaye alisimamishwa kazi miaka minne iliyopita wakati Rais Magufuli akizindua daraja Kigamboni jijini.

Kabwe alisimamishwa kazi baada ya Mkuu wa Mkoa wa wakati huo, Paul Makonda, kulalamika mbele ya Rais kwamba baadhi ya mikataba iliyotiwa saini na Halmashauri ya Jiji hilo kuwa ina matatizo.

Makonda alilalamika uendeshaji wa Kituo cha Mabasi cha Ubungo kwamba una mazingira ya rushwa, jambo ambalo linaiingiza serikali katika hasara kubwa.

Septemba 22, mwaka jana, katika hafla ya kuwaapisha viongozi wapya aliowateua siku mbili nyuma akiwamo Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Sanare, ambaye alichukua nafasi, Dk. Stephen Kebwe, baada ya uteuzi wake kutenguliwa, Rais Magufuli alisema kazi ya kuteua na kutengua viongozi ni kazi yenye machungu.

"Kiukweli kazi ya kuteua na kutengua ni ngumu sana. Kama kuna kazi inayonipa shida sana ni kumteua mtu kisha baadaye unamtengua.

"Ni kazi ambayo ina machungu, lakini saa nyingine inabidi ufanye. Ninamshukuru Dk. Kebwe yupo hapa, lakini ukweli bila unafiki kama kuna mkoa uliotusumbua katika kuongoza ni Morogoro," alisema.

Novemba 10, mwaka 2018, sakata la korosho liliwaondoa kwenye nafasi zao aliyekuwa Waziri wa Kilimo, Charles Tizeba, na aliyekuwa Waziri wa Biashara, Charles Mwijage, baada ya Oktoba 28, mwaka huo Rais Magufuli kufanya mkutano na wanunuzi wakuu wa korosho na kubaini kuwapo kwa dosari ambazo zilipaswa kushughulikiwa na wateule wake. Januari 23, mwaka huu, Rais Magufuli alithibitisha kukubali barua ya kujiuzulu kwa aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, wakati akiwa kwenye hafla ya kukabidhi nyumba za askari magereza Ukonga jijini Dar es Salaam. Rais Magufuli alisema licha ya kuwa rafiki mkubwa wa Lugola, hafai kusalia katika ofisi yake kutokana na makosa aliyoyafanya. "Tuna changamoto nyingi na hasa hii ya mambo ya ndani, kama kuna wizara inanitesa ni Wizara ya Mambo ya Ndani, ninataka muelewe hivyo Watanzania, inatesa sana.

"Katika kipindi cha miaka minne, kuna tume nyingi tu zimeundwa kwa ajili ya kuchunguza Wizara ya Mambo ya Ndani kwa miradi ya ovyo iliyokuwa ikifanyika, na mimi nilitegemea watu watakuwa wanajifunza.

"Ninajua leo waziri wa mambo ya ndani haonekani hapa ameshaleta barua ya kujiuzulu na nimeshamkubalia na ninempongeza kwa hilo," alisema.

Siku hiyo hiyo, Rais Magufuli alitengua uteuzi wa Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Thobias Andengenye, kutokana na mkataba uliotiwa saini na jeshi hilo ambao baadaye kiongozi huyo wa nchi aliagiza uiingie katika uchunguzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Hata hivyo, miezi sita baadaye, Andengenye aliteuliwa na Rais Magufuli kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, ikiwekwa wazi kuwa tayari kiongozi huyo alikuwa ameomba radhi na kujutia makosa yake.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (wa tatu kushoto), akishiriki katika Swala ya Eid El Hajj, iliyofanyika kitaifa kwenye viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam, jana. Wa pili kushoto ni Sheikh Mkuu wa Tanzania Mufti Abubakar Zubeir Bin Ally na wa nne kushoto ni Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Salum. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Majaliwa aonya matamko binafsi

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewataka viongozi wa dini nchini kujiepusha na matamko binafsi yenye lengo la kusababisha vurugu kwenye dini na taifa.

Vilevile, amesema serikali imeunda tume iliyohusisha wakuu wa mikoa kwa ajili ya kuchunguza chanzo cha shule za kiislam nchini kuungua moto.

Majaliwa aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika Baraza la Eid Eladh'haa lililofanyika kwenye Viwanja vya Mnazi Mmoja.

Alisema matamko ya watu binafsi yenye dhana ya kubeba maoni binafsi, kuyachanganya na msimamo wa jumuiya au dini ni jambo linaloweza kusababisha machafuko nchini.

"Wewe peke yako umewaza, kwa utashi wako, ukaenda mbele ukaaminisha kuwa hili tamko ni la wote. Muhimu sana tuwe na tahadhari hiyo," alionya Majaliwa.

Alisisitiza viongozi wa dini kuendeleza mshikamano na taasisi za dini na nyingine za kiraia, ili kuendelea kujenga umoja wa taifa.

"Mheshimiwa Mufti kama kiongozi wetu mkuu, unafanya kazi nzuri sana, umetuunganisha, umetunasihi, usisahau pia kutukemea panapotakiwa kuturekebisha, turekebishe," alisema.

Majaliwa alisema wapo viogozi ambao wanaaminika na jamii na wanapotoa matamko binafsi yanayotaka kuaminisha ni msimamo wa dini ya kiislam na yanaleta taharuki.

Majaliwa alionya kuwa serikali haitawafumbia macho viongozi kama hao ambao wanazungumza mambo ambayo hayapo na yenye mlengo wa kuharibu amani ya nchi.

Kuhusu matukio hayo ya moto, Majaliwa alisema ameshamwagiza Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge, kuunda tume ya kufanya uchunguzi katika shule zote ambazo ziliungua ili kufahamu chanzo chake.

"Tume inakamilisha ripoti ya matukio haya na tutatoa taarifa na serikali haitawafumbia macho watakaobainika walihusika katika matukio hayo ama kwa njama. Na kama ni makosa yalifanyika, tutawaeleza," alisema Majaliwa.

Alisema shule za dini zina maslahi na taifa, hivyo hakuna sababu ya kulifumbia macho suala hilo.

Awali, Mufti Mkuu wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zuberi, alimwomba Majaliwa kusimamia uchunguzi uliofanyika kuhusu kuungua mfululizo kwa shule za dini ya kiislam nchini.

Alisema wanapata shaka kutokana na mazingira ya shule hizo kuungua kwa mfululizo na kwamba wameshindwa kulifumbia macho suala hilo.

"Shule zimeungua saba, hatujui chanzo chake, tumeshtushwa na idadi na mfululizo. Tunapata wasiwasi kwa nini zimeungua kwa wakati mmoja na kwa nini shule hizo tu. Tunaomba tujue tume inayochunguza itupe matokeo ya sababu za kuungua kwa shule hizo," alisema Sheikh Zuber.

**UCHAGUZI HURU**

Katika baraza hilo, Majaliwa pia alisema Rais John Magufuli ameshawahakikishia Watanzania kuwa uchaguzi mkuu uliopangwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu, utakuwa wa huru na haki na hivyo Watanzania wanatakiwa kuamini hivyo badala ya kuendelea kujengeana hofu.

"Uchaguzi wa mwaka huu utakuwa wa huru na wa haki. Kwa hiyo, twende na hilo, tusianze kujengeana shaka, uchaguzi kuwa huru na haki inawezekana na ninawaambia inawezekana," alisema Majaliwa.

Alisema viongozi wa dini wana wajibu wa kuendelea kuliombea taifa ili uchaguzi huo umalizike salama na wajiepushe na lugha za uchochezi.

Aliwasihi wanasiasa kuzungumza hoja za watakachofanya endapo watachaguliwa badala ya kuzungumza matusi na maneno ya kashfa.

Majaliwa alisema katika uchaguzi wa mwaka huu, watu mbalimbali wamejitokeza kuwania nafasi za uongozi bila kuangalia itikadi za kidini.

**HAKUNA CORONA**

Majaliwa pia aliwashukuru viongozi wa dini kwa kuliombea taifa wakati wa ugonjwa wa corona, akiamini maombi yamewezesha kutoweka kwake na kwamba hadi jana hakukuwa na mgonjwa katika hospitali zote nchini.

Alisema Rais Magufuli ndiye aliwatoa hofu Watanzania na viongozi wa dini ambao walishirikiana naye kuondoa hofu iliyokuwa imelikumba taifa.

"Bado kuna mataifa yanaendelea kutikisika, sisi tumepata mgonjwa wa kwanza Machi mwaka huu, tulitikisika kweli kweli na tukaingia kwenye tafrani kwa sababu tu wale wakubwa (nchi zilizoendelea), waliingia kwenye tafrani," alisema Majaliwa.

Alisema Watanzania walijenga hofu nzito kwa sababu ya kujilinganisha na mataifa mengine kiuchumi ambayo yameidizi Tanzania, lakini walizidiwa na ugonjwa huo.

"Viongozi wa dini hatusiti kushukuru na Mwenyezi Mungu alimwongoza Rais Magufuli, kumpa maono na kumwambia atoke hadharani, sema hili, wape faraja Watanzania.

"Alipokuja kutusihi tuwe watulivu, tupunguze hofu na kwamba ugonjwa huu ni wa kawaida. Aliposema tu ni wa kawaida wapo walioelewa na wapo ambao hawakuelewa na nyie viongozi wa dini mlitoka mkamsaidia Rais kuhimiza watu kuondoa hofu," alisifu.

Aliwataka Watanzania kupuuza habari za uzushi kuwa Tanzania kuna corona kwa sababu zina lengo la uchonganishi na mataifa mengine.

Majaliwa pia alisema kwa maombi ya viongozi wa dini, Mungu aliliepusha taifa na majanga ya nzige ambao kama wangeingia nchini, wangesababisha madhara makubwa.

## HABARI KITAIFA



Wasamaria wema wakimsaidia mwendesha bodaboda kunyanyua chombo chake kilichosheheni magunia ya mkaa katika eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam jana. PICHA: NEEMA SIGALIYE - TUDARCO

# Sababu za kuzama boti Ziwa Tanganyika zatajwa

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

SABABU za watu 10 kufa maji na wengine 100 kunusurika baada ya boti waliokuwa wakisafiria kuzama katika Ziwa Tanganyika ni dhoruba kali, imeelezwa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, kamishna Msaidizi (ACP) James Manyama, alisema chanzo cha kuzama na kusababisha ajali ya boti hiyo ni dhoruba iliyotokea wakati chombo hicho kikiwa safarini.

Manyama alisema ajali hiyo ilitokea juzi katika eneo la Sibwesa wilayani Uvinza wakati boti ya abiria iliyokuwa imebeba zaidi ya watu 100 ikitoka eneo la Sibwesa kwenda Mpanda mkoani Katavi kupasuka na kuzama.

Alisema baada ya taarifa za kutokea kwa tukio hilo, takriban watu 100 waliokolewa wakiwa hai katika ajali hiyo na miili ya watu 10 kupatikana. Miongoni mwa miili hiyo, walikuwamo watoto wadogo sita, wanawake watatu na mwanamume mmoja.

Kutokana na tukio huilo, Manyama aliwataka wamiliki wa vyombo vya usafiri majini kuchukua tahadhari zaidi ikiwamo kuahirisha safari pindi wanapoona hali ya hewa ziwani imechafuka. Pia aliwataka kuhakikisha wanabeba abiria kadri ya uwezo wa chombo na maboya ya kutosha. "Wamiliki wa vyombo wanapaswa kuchukua tahadhari zaidi kwa kujua kuwa ziwa Tanganyika lina mawimbi makubwa," alisema.

Pia aliwataka wananchi kukubali kuahirisha safari pindi wanapoona chombo kimejaa ili kunusuru maisha yao kutokana na eneo hilo kutumia usafiri wa maji pekee.

Naye Mganga Mkuu wa Wilaya ya Uvinza, Dk. Reuben Mwakilima, alisema wamepokea miili ya watu 10 katika Kituo cha Afya cha Kalya na majeruhi wa tukio hilo ambao hawakuwa na hali mbaya za kiafya. Alisema baadhi yao walipatiwa matibabu madogo na kuruhusiwa.

Ajali hiyo inakuwa ya pili baada ya kipindi cha mwezi mmoja kupita kwani mwishoni mwa Juni, mwaka huu, watu tisa walikufa maji kutokana na chombo walichokuwa wakisafiria kuzama.

# Akemea vurugu uchaguzi mkuu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

SHEIKH Balilusa Khamis wa mjini Shinyanga, amewataka viongozi wa vyama vya kisiasa nchini na wanachama wao, kutanguliza mbele maslahi ya taifa na kutofanya vurugu wakati wa uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Alitoa rai hiyo jana baada ya kuongoza ibada ya sikukuu ya Eid Al Hajj iliyofanyika kwenye Uwanja wa Uhuru mjini hapa, akibainisha kuwa, matarajio ya viongozi wa dini ni kuona uchaguzi huo unakuwa huru na utulivu unakuwapo.

Sheikh Khamis ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Amani Mkoa wa Shinyanga, alisema viongozi wa siasa na wanachama wao, wanapaswa kutanguliza maslahi ya taifa mbele na siyo maslahi yao binafsi katika kipindi chote cha uchaguzi huo.

"Sisi kama viongozi wa dini, tunawaomba sana viongozi wa kisiasa hapa nchini pamoja na wanachama wao, katika kipindi hiki cha kuelekea kwenye uchaguzi mkuu, watanguliże maslahi ya taifa na siyo maslahi yao binafsi, ili kulinda amani ya nchi yetu na kutofanya vurugu zozote kwenye uchaguzi," alisema.

Shekh Khamis pia aliwataka wakuu wote wa shule binafsi kutowanyima wanafunzi muda wa kwenda kusali, kwa madai ya kufidia muda uliopotea wakati wa likizo ya lazima kupisha corona.

Mjumbe wa Baraza la Masheikh mjini Shinyanga, Sheikh Khalfan Ally, akitoa mawaidha, aliwataka waumini wa dini ya Kiislam hasa vijana, kuzingatia miiko na sheria ya dini hiyo, ili kutoporomoka kimaadili na kuacha kuzaa watoto kabla ya kufunga ndoa.

Alisema baadhi ya vijana wa dini hiyo hawana maadili kabisa, ambapo wamekuwa wakifanya uzinzi na kuzaa nje ya ndoa, kutovaa mavazi ya heshima, kunyoa mitindo ya ovyo ya nywele na kupenda maisha rahisi kwa kuoa wanawake wenye pesa.

# 'Mkapa alifanikisha Msikiti wa Gaddafi'

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SHEIKH wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, amesema atamkumbuka kwa mambo mengi mazuri Rais Benjamin Mkapa, ikiwa ni pamoja na namna alivyofanikisha ujenzi wa Msikiti wa Gaddafi jijini Dodoma.

Akizungumza jana jijini Dodoma wakati wa ibada ya Eid El Hajj iliyofanyika katika msikiti huo, Sheikh Rajabu alisema Mkapa aliyezikwa Jumatano wilayani Masasi mkoani Kilimanaro, alikuwa kiongozi mwadilifu na msikivu kwa mkubwa na mdogo.

Sheikh Rajabu alisema alionana na Rais Mkapa Libya na kufanikisha ujenzi wa msikiti huo wa kisasa na atamkumbuka kiongozi huyo wa nchi kwa jambo hilo muhimu kwa waumini wa dini ya Kiislamu.

"Taifa limepata msiba mkubwa wa aliyekuwa Rais wa awamu ya tatu, Benjamini Mkapa. Pamoja na imani yake, amefanya mengi ambayo ni ya kukumbukwa, alikuwa muungwana sana," alisema.

Sheikh Rajabu alisema kuwa alikutana na Mkapa nchini humo miaka kadhaa iliyopita wakati huo yeye alikuwa akisoma na Rais Mkapa alifika kwa ajili ya kuiomba Serikali ya Libya kuwajengea Tanzania msikiti wa kisasa.

Alisema Mkapa alifika Libya akiwa na maombi ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma wakati huo, Mussa Nkangaa, kwa Serikali ya Libya wajengewe msikiti wenye hadhi.

"Tulikuwa vijana kadhaa ambao tulikuwa tukisoma kule Libya, tulienda mpaka katika hoteli ambayo alifikia, na tulikutana naye. Alishangaa kutukuta kule huku akisema yeye haelewi kitu kwani kila kitu kimeandikwa kiarabu.

"Alipoitwa kwamba tumefika, alishangaa kusikia kuna watanzania kule, lakini alishuka na tulizungumza naye kwa kirefu, hakika alikuwa ni muungwana, alipeleka ule ujumbe na Libya wakakubali kujenga msikiti huu ambao ndiyo tunaswali hapa," alisema.

Alisema wakati msikiti unakaribia kukamilika, Mkapa alifika na kukagua na hakuridhishwa na sehemu ya kunawia kwa kuwa ilikuwa juu, hivyo aliagiza ivunjwe.

"Hakuridhishwa na ile sehemu, akaagiza kuvunjwa, alisema mtu mfupi kama yeye atachukuaje udhu katika sehemu ambayo ipo juu vile, hivyo tulijenga kwa chini kidogo na sehemu za kukaa kwa kila mtu wakati akinawa," alisema.

"Mkapa alikuwa na mambo mengi sana, leo tunayaona na kusema sababu ameishafariki dunia. Mimi ninasema akiwa hai Rais wetu Magufuli ametupigania sana sisi Waislamu na ndiyo maana sasa unajengwa ule msikiti mkubwa jijini Dar es Salaam, anachapa kazi iliyotukuka."

**CHUO KIKUU MOROGORO**

Alisema jambo la pili ambalo analikumbuka kwa Mkapa ni kutoa jengo la umma la Shirika la Umeme (TANESCO) mkoani Morogoro na kuwapa waislamu ili kiwe Chuo Kikuu cha Kiislamu.

Alisema jambo hilo limeendelea kubaki katika kumbukumbu yake kwa kuwa Mkapa alikutana na wakati mgumu wakati watu walipohoji sababu ya kutoa mali ya umma kwa Waislamu.


## IBADA YA SHUKRANI

*"Kama Kristu alivyokufa na kufufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye" 1 The 4:14.*



ABRAHAM GEORGE MISSANGA

Familia ya Marehemu **Mr & Mrs Fredrick G.M ALI** wa Yombo Machimbo, tunapenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zetu za dhati kwa ndugu, jamaa, marafiki na majirani wote kwa msaada wenu wa hali na mali mlioutoa katika kufanikisha msiba na mazishi ya **ABRAHAM GEORGE MISSANGA** aliyeitwa na Mungu **tarehe 11 Juni, 2020** katika Hospitali ya **SUNA HEALTH CENTRE.**

Tunapenda kutoa shukrani maalumu kwa Wizara ya TAMISEMI hasa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga kwa ushirikiano wao.

Shukrani pia ziwaendee Mapadre wa Parokia ya Mtakatifu Theresia mtoto wa Yesu Dar es salaam na Parokia ya Puma Singida, Jumuiya ya Mtakatifu Anyesi ya Yombo Machimbo na waumini wote.

*Aidha tunapenda kuwaalika ndugu, jamaa, marafiki na waumini wote katika ibada ya shukrani itakayofanyika katika kanisa la Mtakatifu Theresia Mtoto wa Yesu Dar es salaam. Ibada hiyo itafanyika siku ya Jumapili ya tarehe 02/08/2020. Ibada itatanguliwa na mkesha na maombi yatakayofanyika nyumbani, mtaa wa Yombo Machimbo tarehe 01/08/2020. KARIBUNI WOTE.*

**"Heri wenye moyo safi maana watamuona Mungu" Mt. 5:8.**



Baadhi ya waumini wa kanisa la Christ Embassy Church Mbezi Makonde, wakijitolea kuchangia damu kuadhimisha Siku ya kuchangia Damu Duniani, iliyofanyika kanisani hapo, jijini Dar es Salaam juzi. Anayewahudumia ni mtaalamu kutoka Damu Salama, Dk. Peter Chami. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# CHADEMA yatamba kuibuka na ushindi Kyela

**Na Mwandishi Wetu,** KYELA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimetamba kuibuka na ushindi katika Jimbo la Kyela mkoani Mbeya katika uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba, mwaka huu.

Mshindi wa kura za maoni ndani wa CHADEMA katika jimbo hilo, John Mwalwande, akizungumza katika mahojiano na gazeti hili jana, alisema chama hicho kimejipanga na kuibuka na ushindi katika majimbo kadhaa likiwamo jimbo la Kyela.

"Kyela ni moja ya majimbo ya mkoa wa Mbeya ambayo tuna uhakika wa kunyakua kiulaini katika uchaguzi mkuu mwaka huu," alisema Mwalwande.

Alitaja sababu zinazowapa uhakika wa kushinda katika uchaguzi huo ni pamoja na changamoto za barabara, maji, elimu na mahitaji mengine ya kijamii ambayo alidai kuwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimeshindwa kuzitatua.

Alisema kinachowapa uhakika wa ushindi katika uchaguzi huu ni mfumo mzima ndani ya CCM katika kupata watia nia ambapo baadhi walitumia rushwa ili kujihakikishia ushindi. "Mfano wagombea walioshika nafasi ya juu katika kura za maoni ndani ya CCM walikuwa viongozi ndani ya wilaya. Mmoja ni Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya Kyela na mwingine Mwenyekiti wa Halmashuari. Wote hao wameshinda kutatua kero za wananchi, hivyo hii inatupa nafasi ya kushinda,' alisema.

Pia alisema viongozi hao wanatuhimiwa kushiriki kupora mashamba ya mpunga ya wananchi kwa matumizi binafsi jambo ambalo limewaudhi wananchi.

Kuhusu tuhuma za rushwa wakati wa kura za maoni ndani ya CCM, mgombea huyo wa CHADEMA alisema zimeibua wagombea dhaifu kupambana na chama hicho.

"Kutoa rushwa kwa wajumbe wa chama chao haiwezi kuwapa tathimini nzuri ya kupendwa na wananchi bali ni kujidanganya na hii ni tufuru nzuri kwa Chadema, " alisema.

Mwalwande alisema uchaguzi mwaka huu wananchi wa jimbo la Kyela wategemee mabadiliko ya uwajibikaji kwa chama tawala kukaa pembeni na Chadema kutawala na kuleta fikra mpya za maendeleo.

Naye mwanachama wa CCM kata ya Makwale, Sisita Malundi, alisema matamshi holela ya watia nia wa CCM kwamba hakuna maendeleo yaliyofanyika, yamewaweka wanaCCM kwenye hali mbaya ya kujibu mashambulizi ya upinzani. "Haiwezekani wewe ni kiongozi ndani ya chama ukasema hakuna maendeleo yaliyofanyika ili kujenga hoja uchaguliwe kwenye kura za maoni. Sasa tunajiuliza hao waliochaguliwa watawajibu nini wananchi kwenye uchaguzi," alisema.

Mwanachama mwingine kutoka Kata ya Ipinda, Benjamini Mwakalebela, alisema matamshi yetu wenyewe wana CCM yamegeuka kuwa mtaji kwa wapinzani.

# Meneja TANROADS Lindi atumbuliwa

**Na Romana Mallya**

BAADA ya Rais John Magufuli kueleza kukerwa na ubovu wa barabara Mtwara-Lindi, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, ametengua uteuzi wa Meneja wa TANROADS Mkoa wa Lindi, Isack Mwanawima.

Uteuzi wa Mwanawima alitenguliwa juzi ikiwa ni saa chache baada ya msafara wa Rais Magufuli kusimama eneo la Somanga, Kilwa mkoani Pwani, na kuwaeleza wananchi kuwa amepata uchungu kutokana na ubovu wa barabara hiyo.

Rais Magufuli alikuwa njiani kwenda Dar es Salaam akitokea Lupaso, Masasi mkoani Mtwara alikokwenda kuongoza maziko ya Rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa.

Alipofika Somanga Rais Magufuli alisema amepata uchungu wa kumzika Mzee Mkapa na mengine kutokana na ubovu wa barabara hiyo.

"Nimepata machungu mengine humu barabarani kwa kukuta barabara haijatengenezwa hata visehemu vidogo vidogo wameshindwa kukarabati, hili mniachie nitalishughulikia," alisema.

Baada ya muda mfupi, Waziri Kamwelwe kupitia taarifa yake, alisema Rais Magufuli ameshuhudia ubovu mkubwa wa barabara kipande cha Nangurukuru-Mbwemkuru chenye urefu wa kilometa 90.

Waziri huyo alitangaza kutengua uteuzi wa meneja huyo kwa kuwa alishawahi kutoa maelekezo kwa mameneja wa mikoa wa TANROADS kuhakikisha barabara wanazozisimamia zinakuwa na hali nzuri na zinapitika vizuri wakati wote. "Ninamwagiza Mtendaji Mkuu wa TANROADS apelike mhandisi mwingine haraka kwa ajili ya kuimarisha usimamizi na kufanyia matengenezo barabara hiyo haraka," aliagiza.


BANK OF AFRICA
Groupe BMCE BANK

## TAARIFA KWA WATEJA

Wateja wetu wapendwa na wadau wa BANK OF AFRICA,

Kama sehemu ya mkakati wa benki kuboresha huduma, inayoongozwa na mikakati ya kidigitali.
Tunapenda kuwajulisha kwamba, kuanzia tarehe 01/09/2020, tutaunganisha baadhi ya matawi yetu; Matawi yataungana kama ifuatavyo;

- Tawi la Mtoni lililopo Mtoni Mtongani, litaunganishwa na Tawi la Tandika
- Tawi la Babati litaunganishwa na Tawi la Arusha
- Tawi la Mbezi Louis lililopo Soko la Mbezi Louis, litaunganishwana Tawi la Sinza
- Tawi la Mwenge, litaunganishwa na Tawi la Victoria

Zoezi hili halitaathiri huduma kwa wateja wetu,

BANK OF AFRICA imejipanga kikamilifu katika uwekezaji ndani ya Tanzania, ikiwemo kutoa huduma mbalimbali katika makundi ya wateja wa rejareja, wafanya biashara wadogo na wakati na wateja wa makampuni. Wateja wetu bado wanaweza kufurahia huduma zetu zinazopatikana kupitia matawi yaliyopo karibu yao na mifumo ya kidigitali (Benki kwa njia ya Simu ya Mkononi, Benki kwa njia ya Mtandao na ATM).

**Tangazo hili limetolewa na Uongozi wa BANK OF AFRICA**

Kwa mawasiliano zaidi tembelea, website www.boatanzania.com


# Waziri ampa kibano mkurugenzi malipo ya korosho

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, ametoa siku 14 kwa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CBP), Dk. Anslem Moshi, kukamilisha malipo ya wakulima wote waliouza korosho msimu wa mwaka 2018/19.

Hasunga alitoa agizo hilo jana alipotembelea na kukagua shughuli za utendaji kazi zinazofanywa na bodi hiyo jijini hapa.

Alisema bodi hiyo ilipewa dhamana ya kununua korosho mwaka 2018 kwa niaba ya serikali na tayari serikali imeshatoa fedha zote kwa ajili ya wakulima lakini haijakamilisha malipo, hivyo ni lazima itekeleze agizo hilo ndani ya siku hizo.

"Ndani ya siku 14 sitaki kusikia malalamiko ya wakulima. Lazima wakulima wote wawe wamelipwa fedha zao haraka iwezekanavyo," alisisitiza. Hasunga alimwagiza mkurugenzi huyo kuwasilisha haraka mpango kazi wa namna viwanda vitakavyofanya kazi kwa ajili ya kutengeneza bidhaa zitakazohitajika na wateja na kukidhi matarajio ya serikali ikiwa ni pamoja na kuainisha idadi ya watumishi wanaohitajika.

Hasunga aliiagiza kampuni ya Monaban ambayo ilikuwa imekodi kiwanda cha nafaka kutekeleza maagizo ya serikali yaliyotolewa mwaka jana ya kuhamisha mali zao zote zilizoko katika eneo hilo la serikali kwa kuwa kesi mahakamani na notisi ilishaisha.

Akiwa kiwandani hapo, Waziri Hasunga alibaini uchakavu wa mitambo iliyopo pamoja na uchache wa watumishi wanaofanya kazi, hivyo kuagiza kufanyika ukarabati wa majengo kuanzia mwezi huu badala ya Oktoba, mwaka huu, kama kampuni hiyo ilivyopanga.

"Tukisubiri mpaka mwezi wa kumi tutakuwa tumechelewa kwa kuwa mvua zitaanza kunyesha jambo ambalo litasababisha kushindikana kufanyika ukarabati," alisema.

Hasunga alisema lengo la serikali ni kufufua viwanda kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao ya nafaka nchini ili kuzalisha bidhaa mbalimbali kama unga na kuuza katika masoko ya ushindani ndani na nje ya nchi.

HABARI KITAIFA



Mratibu wa utafiti wa zao la viazi mviringo kitaifa ambaye pia ni Mtafiti Mkuu wa Kilimo Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI), Kituo cha Uyole, Dk. Juma Kayeke, akiwaonyesha waandishi wa habari, kituoni hapo, jijini Mbeya jana, mbegu za viazi ambazo zitatumika katika maonesho ya Nane Nane, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, ambayo yatafanyika kwenye Viwanja vya John Mwakangale Mbeya. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# PASS kuwezesha mikopo 1,260,000 wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Asasi ya PASS, umesema unajivunia kusaidia ukuaji wa sekta ya kilimobiashara nchini tangu kuanzishwa kwake mwaka 2000, ikiwezesha upatikanaji wa mikopo ya mabilioni ya shilingi kwa wajasiriamali katika sekta hiyo.

Vilevile, asasi hiyo iliyoanza kazi zake rasmi nchini mwaka 2007 kwa lengo la kuwezesha maendeleo ya wajasiriamali katika sekta ya kilimobiashara, imepanga kuwezesha mikopo 1,267,800 kwa wajasiriamali katika sekta hiyo kufikia mwaka 2022.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa PASS, Nicomed Bohay, asasi hiyo katika kutekeleza majukumu yake, imekuwa ikishirikiana benki 13 zikiwamo CRDB, Akiba, BoA, Amana, NBC, Equity, Mkombozi, Access, Azania, TPB, na TADB.

Bohay alibainisha jana kuwa katika robo ya kwanza ya mwaka huu (Januari hadi Machi 2020), mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 71.5 ilikuwa imetolewa kwa wajasiriamali kwa udhamini wa PASS.

Alisema kuwa, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2000 hadi Machi 31 mwaka huu, jumla ya miradi 36,007 yenye thamani ya Sh. bilioni 916.4 ilikuwa imeidhinishiwa mikopo kwa udhamini wa PASS, ikihusisha wajasiriamali 1,196,891 walionufaika.

"Inafurahisha zaidi kwamba kati yao, asilimia 45 ni wanawake. Wajasirimali hawa ni wakulima, Vyama vya Kuweka Akiba na Kukopa (SACCOS), mashirika na vyama vya wakulima, kampuni na mjasiriamali mmoja mmoja anayejihusisha na kilimobiashara," alisema.

Bohay alibainisha kuwa, licha ya mlipuko wa corona uliokuwa tishio zaidi Januari na Machi mwaka huu, PASS imewezesha kuanzishwa kwa miradi 4,404 yenye mikopo kwa wanufaika 41,030 (asilimia 65 wakiwa ni wanaume).

Takwimu za Benki Kuu (BoT) mwaka huu zinaonyesha PASS imetoa mchango mkubwa katika sekta ya kilimo nchini. Kwa mujibu wa BoT, kati ya mikopo 8,285,831 iliyotolewa na benki kwa sekta ya kilimo nchini kati ya mwaka 2013 na Novemba 2019, mikopo 956,298 ilidhaminiwa na PASS.

Bohay alisema kuwa, katika kuunga mkono jitihada za serikali katika kukuza uchumi wa nchi, PASS katika mikakati yake ya mwaka 2018-2022, imepanga inawezesha mikopo walau 1,267,800 kwa wajasiriamali katika sekta ya kilimobiashara na kupunguza tatizo la ajira nchini.

"Pia tumepanga kuongeza kiwango cha mikopo tunayoidhamini kutoka Sh. bilioni 126 kwa mwaka (2018) hadi kufikia Sh. bilioni 184 mwaka 2022 na kutoa mikopo zaidi kwa wajasiriamali wanawake," alisema.

Alisema malengo mahususi kwa mwaka huu (2020) ni kuyafikia makundi muhimu hasa kuwawezesha vijana na wanawake kujikwamua kiuchumi kupitia kilimobiashara.

# Tanzania yapiga hatua kilimo cha mboga

**Na Renatha Msungu,**
ARUSHA

TANZANIA imepiga hatua katika kilimo cha mboga baada ya kufanikiwa kuongeza aina 19 za mbegu za mbogamboga na viungo, watafiti wamebaini.

Wataalamu hao pia wamesema Tanzania iko mbioni kuikamata Kenya katika uzalishaji wa bidhaa hiyo, wakibainisha kuwa takwimu za sasa zinaonyesha Tanzania inapata Sh. milioni 800 kwa mwaka wakati Kenya wanakusanya Sh. bilion moja kutokana na kilimo hicho.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika wa Kituo cha Utafiti wa Mbegu za Mboga, Dk. Gabriel Rugalema, alisema mbegu hizo zimeonyesha kuwa na soko kubwa duniani.

Alisema aina hizo za mbegu zinaoteshwa katika vitalu kwenye bustani yao na zinauzwa kwa wakulima mbalimbali nchini na nje ya nchi.

Dk. Rugalema pia alisema wamekuwa wakitoa mafunzo kwa wakulima wanaopata mbegu, akibainisha kuwa wateja wao hao wamegawanyika katika makundi matatu, likiwamo la wanafunzi kutoka vyuo mbalimbali nchini.

Alibainisha kuwa wakulima hao ni kutoka mikoa ya Mtwara, Manyara, Kilimanjaro, Moshi, Arusha na Zanzibar.

Dk. Rugalema alisema kituo cha uzalishaji mboga cha jijini Arusha kina fursa ya kufundisha vikundi namna ya utunzaji mbegu ili kuwapa manufaa katika kilimo wanachofanya.

"Tumekuwa tukifundisha watu ili kuhakikisha kila kitu kinaenda sawa, tunafanya jitihada za kuinua kilimo cha mbogamboga na viungo," alisema Dk. Rugalema.

Aliishukuru serikali kwa kuwaongeza mkataba wa kuendelea kuwa nao, akiahidi kupanua zaidi huduma zao.

Mkulima Gilbert Mushi alisema kituo hicho kimekuwa msaada mkubwa kwao kutokana na kuwapa elimu kuhusiana na kilimo cha mbogamboga.

"Tunakishukuru kituo hiki kwa kututoa kwenye kilimo cha hasara na kutuingiza kilimo cha faida, tunaona matunda yake, " alipongeza mkulima huyo.

# TARI kugawa bure mbegu Nanenane

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Kituo cha Uyole, inakusudia kutoa bure mbegu za mazao ya aina mbalimbali kwa wakulima watakaotembelea banda lake kwenye viwanja vya maonyesho ya kilimo maarufu Nanenane, jijini Mbeya, ili kuwajengea wananchi utamaduni wa kutumia mbegu za kisasa.

Ofisa Ughani wa taasisi hiyo Kituo cha Uyole, Nyimila Kalindile, alitangaza neema hiyo kwa wakulima alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya mwisho ya banda la maonyesho la taasisi hiyo.

Alisema wameamua kufanya kwa lengo la kuhamasisha wakulima kutembelea taasisi hiyo na kujifunza teknolojia na elimu ya kilimo bora.

"Mwaka huu katika maonyesho ya Nanenane tunatoa ofa kwa wakulima ambao watatembelea banda letu la TARI Uyole kupewa mbegu za maharage ili kwenda kufanya majaribio na kuona ubora wake," alisema Kalindile.

Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema taasisi hiyo imeongeza idadi za mbegu mpya za mazao ya aina mbalimbali ambazo zitaonyeshwa kwa wananchi kwa mara ya kwanza wakati wa maonyesho ya kilimo ya mwaka huu ambayo yanaanza leo kwenye Viwanja vya John Mwakangale jijini.

Alisema mbegu hizo ambazo zimebuniwa na kituo hicho, zina ubora na zitaongeza uzalishaji kwa mkulima, hivyo akawahamasisha kujitokeza kwa wingi kujifunza maarifa na teknolojia mpya.

Baadhi ya watafiti walisema mbali na uwepo wa mbegu mpya za mazao, pia wameandaa teknolojia mpya na za kisasa ambazo kumwezesha mkulima mdogo kuachana na kilimo cha mazoea na kuanza kilimo kisasa.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Klabu zitangulize maslahi ya wachezaji dirisha hili

**RASMI** dirisha kubwa la usajili kwa klabu za Tanzania Bara kuelekea msimu ujao limefunguliwa leo Agosti Mosi na litadumu hadi mwishoni mwa mwezi huu, kabla ya msimu mpya kuanza katikati ya mwezi ujao.

Kufunguliwa kwa dirisha hilo ni nafasi pekee kwa klabu husussan za Ligi Kuu, Daraja la Kwanza na la Pili kuboresha vikosi vyao ama kuvisuka upya kabla ya msimu mpya kuanza.

Tayari baadhi ya klabu zimeshaanza kuhusishwa na wachezaji kadhaa kutoka ndani na nje huku wengine wakifunguliwa milango ya kutokea kwa klabu zao kutangaza hazitahitaji huduma zao msimu ujao.

Hata hivyo, tunatambua katika dirisha hili kama yalivyo mengine, wapo wachezaji wataachwa kutokana na mikataba yao kumalizika ama watatemwa kwa sababu ya viwango vyao kushuka, ili kutoa nafasi kwa nyota wapya ambao klabu husika zinaamini wanaweza kuzisaidia kutimiza malengo yao ya msimu ujao.

Lakini kutemwa kwao hakuwezi kuwa safari ya mwisho kwao kisoka kwani upo msemo wa wahenga usemao "ukisema wa nini, mwenzako anajiuliza atampata lini" na unaweza kuonekana hufai hapa ila kwingineko ukawa lulu.

Katika hilo, tunaushahidi wa kutosha kwa baadhi ya wachezaji ambao wamewahi kuonekana hawafai na kutemwa, lakini baada ya kwenda kwingineko wakang'ara na baadaye kusajiwa tena na klabu zilizowatema awali, hivyo kutufanya kuendelea kuamini "kumpiga chura teke ni kumuongezea mwendo".

Kwa mantiki hiyo, wachezaji watakaotemwa hawana budi kutambua hayo ndiyo maisha ya soka na kinachotakiwa ni kupambana zaidi kwa klabu mpya zitakaowasajili ili kuthibitisha ubora wao.

Aidha, tunafahamu wazi zipo klabu ambazo zimetega mitego yao zikisubiri wachezaji watakaotemwa hususan kutoka kwa klabu kubwa ili ziwasajili jambo ambalo Nipashe tungependa kuona klabu zote zikitangulia kwanza kutangaza wachezaji zinaowatema kabla ya kuanza kusajili wapya ili kuwapa fursa ya kujiweka sokoni mapema.

Hatutarajii kuona wachezaji wakutemwa katika dirisha hili wakiwa wa mwisho kutangazwa baada ya klabu husika kufanya usajili kwa kuwa kufanya hivyo ni kutowatendea haki.

Lakini pia kufunguliwa kwa dirisha hili kubwa ni wakati muafaka kwa wachezaji ambao walikuwa hawapati nafasi katika vikosi vya kwanza kuomba kuondoka ili kuokoa viwango vyao na vipaji kwa ujumla.

Tunatambua wapo wachezaji ambao walishawishika kusajiliwa na baadhi ya klabu kutokana tu na kuahidiwa dau kubwa ama kufuata mapenzi yao kwa klabu, na baadaye kujikuta wakisugua benchi katika kila mechi ama kuishia kupata nafasi chache dimbani wakitokea benchi.


Hivyo, wachezaji kama hawa, hawana budi kuomba kuondoka ama kutolewa kwa mkopo badala ya kuendelea kusugua benchi ama kusubiri kucheza wakitokea benchi katika kila mechi jambo ambalo linashusha viwango vyao.

Hivyo, hatutarajii kuona kunakuwa na klabu zitakazowabania wachezaji ambao hawapati nafasi wakitaka kuondoka ama kuwatoa kwa mkopo kama wanamalengo nao kwa baadaye.

Tunayasema hayo kutokana na kutambua kuwa soka kwa sasa ni biashara na ajira kubwa na kwa wachezaji hiyo ni sehemu ya maisha na ndiyo kila kitu kwao katika kuendesha maisha yao ya kila siku.

Lakini pia, matarajio yetu ni kuona usajili wa dirisha hili kanuni na sheria zikifuatwa hasa wachezaji kuepuka kujisajili mara mbili, lakini kwa klabu zikitanguliza mbele maslahi yao kwa kuwasikiliza maoni yao hususan wale wasiopata nafasi katika kikosi cha kwanza.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kitema kuni temato

Na Barnabas Maro

**'TEMATO'** ni tema vizuri. Maana yake ukiamua kuchanja kuni zichanje vizuri. Methali hii yatufunza kuwa tuamuapo kufanya jambo lazima tufanye vizuri na kwa njia iliyo bora zaidi. Matumizi ya kiisho'to' hupatikana katika lugha ya kishairi.

Kadhalika, twakumbushwa na wahenga kuwa "Kilemba hakimfanyi mstaarabu mtu." Maana yake mtu hawezi kuwa mstaarabu kwa kuwa kavaa kilemba. Heshima au taadhima ya mtu pamoja na thamani yake haitokani na sura zake za nje au anavyoongea mbele za watu bali na tabia zake.

Kocha Mbelgiji Luc Eymael alipokewa kwa shangwe na viongozi, pamwe wana Yanga alipotua klabuni. Viongozi, wanachama na mashabiki walitegemea kumwona akibadili kabisa timu yao na kuiwezesha kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu msimu uliomalizika hivi karibuni lakini alishindwa. Simba ndio iliyotwaa Kombe hilo kwa mara ya tatu mfululizo. Sikuona mafanikio yoyote kwenye timu ya Yanga iliyokuwa chini ya mwalimu Luc Eymael anayesemekana kuwa na ubaguzi wa rangi na wachezaji, hata kuwatukana!

Matokeo yake ikawa haelewani na wasaidizi wake aliowakuta hata kusababisha timu kucheza chini ya kiwango, hivyo kila ilipocheza, ilipata ushindi kiduchu (-enye kuwa na kiwango cha chini) tena wa kubahatisha! Wanachama na mashabiki wengi wa Yanga walikata tamaa kwenda kuishangilia kila ilipocheza.

Aidha, ilidhaniwa kuwa usajili wa Mghana Bernard Morrison ungeisaidia sana Yanga katika eneo la ushambuliaji, lakini baada ya kusifiwa sana kwa namna alivyolichezea gozi la ng'ombe, alifura kichwa akidhani yeye ni bora zaidi, si kwa wachezaji wenziwe tu bali hata kwa makocha na viongozi! Akawa hajali maonyo aliyopewa. Yasemekana kuwa hata Afrika Kusini haimtaki Morrison kutokana na tabia zake mbaya. Yanga inasubiri nini kumfukuza ili aende anakotaka?

Ndio maana wahenga walisema: "Kijumba cha ufisadi mbele kina sumbuko." Maana yake mahali panapofanyiwa maovu huwa hapana mwisho mwema. Methali hii hutumiwa kutufunza kuwa tabia mbaya au isiyoelekea huwa haina mwisho mzuri. Mtu mwenye matendo yasiyofungamana na matakwa ya jamii hana mwisho mwema.

Hii ni methali ya kuwazindua watu. Methali hii inawahusu viongozi wa Yanga.

Huyo Morrison atambue kuwa wahenga walikuwa na hekima walipotuachia methali isemayo: "Umejigeuza chachandu (aina ya samaki) kujipalia makaa." Maana yake umejifanya chachandu kuishia kujivutia makaa na kujichoma. Msemo huu hutumiwa kumpigia mfano mtu anayejitosa taabani kutokana na matendo yake mwenyewe.

Hakika kila nilipoiona Yanga ikicheza, iliniwia vigumu kusema ndio timu iliyotwaa Kombe la Ligi Kuu ya Tanzania Bara mara 27 ikifuatiwa na Simba iliyotwaa ubingwa huo mara 21. Simba, wakati ule ikiitwa Sunderland, ilikuwa ya kwanza kutwaa kombe hilo Ligi ilipoanzishwa mwaka 1965 ikitwaa kombe mara mbili mfululizo, yaani msimu wa mwaka 1965 na 1966 ikifuatiwa na timu iliyokuwa machachari, Cosmopolitan pia ya Dar es Salaam mwaka 1967. Baada ya hapo Yanga ilizinduka na kutwaa kombe hilo mara tano mfululizo, mwaka 1968, 1969, 1970, 1971 na 1972.

Timu ya Mseto kutoka Morogoro ilitwaa ubingwa mwaka 1975 kisha Simba ikaijibu Yanga kwa kutwaa kombe hilo mara tano mfululizo, yaani mwaka 1976, 1977, 1978, 1979 na 1980. Kunako mwaka 1981 Yanga ikatwaa kombe hilo, lakini kutokana na mgogoro uliozuka klabuni ikapokonywa na Pan Africans mwaka 1982 baada ya mfarakano, lakini Yanga ikajibu mapigo kwa kulitwaa tena mwaka 1983. Simba ikaipokonya Yanga kombe mwaka 1984 na Yanga kulitwaa mwaka 1985.

Mwaka 1986 Tukuyu Stars ya Mbeya ikatwaa kombe hilo kisha Yanga ikalitwaa tena mwaka 1987. Coastal Union ya Tanga ikalitwaa kwa mara ya kwanza na ya mwisho mwaka 1988 kisha Yanga ikalitwaa tena mwaka 1989. Hata hivyo, Simba ikaipokonya Yanga mwaka 1990 lakini Yanga ikalitwaa tena Kombe kwa miaka mitatu mfululizo 1991, 1992 na 1993.

Simba ilitwaa tena kombe hilo kwa misimu miwili, yaani mwaka 1994 na 1995 kisha kupokonywa na Yanga kwa miaka mitatu 1996, 1997 na 1998. Timu ya Mtibwa Sugar ilitwaa kombe hilo misimu miwili ya mwaka 1999 na 2000 na kutwaliwa tena na Simba mwaka 2001 kisha Yanga mwaka 2002 na Simba kuipokonya Yanga mwaka 2003 na 2004.

Mwaka 2005 na 2006 ikawa zamu ya Yanga kulitwaa na kupokonywa na Simba mwaka 2007, lakini mwaka 2008 na 2009 Yanga ikatwaa tena kombe hilo. Kuanzia hapo ikawa ni kupokezana kwani Simba ililitwaa mwaka 2010 kisha Yanga mwaka 2011, Simba mwaka 2012, Yanga mwaka 2013. Azam nayo ikatwaa kombe hilo mwaka 2014 kisha Yanga ikalitwaa mara tatu mfululizo mwaka 2015, 2016 na 2017 kisha Simba nayo imelitwaa Kombe hilo mfululizo tangu mwaka 2018 mpaka sasa 2020.

## HABARI PICHANI

# SHEREHE ZA EID EL HAJJ KATIKA PICHA



Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, baada ya kumalizika kwa Baraza la Eid El Hajj katika ukumbi wa mitihani wa Shule ya Sekondari Bumbwini, wilaya ya Kaskazini (B), mkoa wa Kaskazini Unguja jana. **PICHA: OMR**



Imamu wa Msikiti wa Nughe, Omari Salumu, akitoa hotuba baada ya Swala ya Eid El Haji, katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Waumini wa dini ya Kiislam wilayani Muheza, mkoani Tanga, wakisalimiana kabla ya kuingia swala ya Eid El Hajj, katika msikiti mkuu wa Ijumaa, jana. Kushoto ni Katibu wa CCM wa wilaya hiyo, Muheza Mohamed Moyo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Waumini wa dini ya Kiislam, wakiwa kwenye swala ya Eid El Hajj, katika uwanja wa Uhuru mjini Shinyanga, jana. **PICHA: MARCO MADUHU**



Waumini wa dini ya Kiislamu wakichinja wanyama ikiwa ni mmoja ya masharti ya kutekeleza kwenye sikukuu ya Eid El Hajj, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Mfanyabiashara wa kuku wa kienyeji (katikati), akipatana bei na mteja wake katika eneo la Buguruni, jijini Dar es Salaam jana. Kuku mmoja aliuzwa kwa bei ya 20,000/-. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Viwanda 30 vya dawa kujengwa

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), inatarajia kuwa na viwanda 30 vya kutengeneza dawa na vifaa tiba nchini katika kutekeleza sera ya kukuza uchumi wa viwanda.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Adam Fimbo, alibainisha hayo juzi wakati wa kikao kazi na waandishi wa habari wa mikoa ya Dar es Salaam na Morogoro kilichohusu usimamizi wa sheria ya dawa na vifaa tiba sura ya 19.

Alisema katika kipindi cha miaka mitano, kumekuwa na ongezeko la wawekezaji wanaoomba kuanzisha viwanda vya dawa na vifaa tiba nchini.

"Takwimu za nyuma zinaonyesha Tanzania inaingiza zaidi dawa na vifaa tiba kuliko zile zinazozalishwa nchini. Inaonekana asilimia 10 tu ya dawa na vifaa tiba ndiyo inazalishwa nchini, asilimia 90 tunaagiza, lakini hii ni kwa mujibu wa utafiti uliofanyika mwaka 2016," alisema Fimbo.

Alisema uwekezaji katika sekta ya afya umekua na kwamba utafiti utakaofanyika tena, hali itakuwa tofauti kwa sababu hadi sasa nchini kuna viwanda 14 na viwanda 16 vipo katika hatua za mwisho kukamilika ujenzi ili kuanza uzalishaji.

Awali, akiwasilisha mada ya mchango wa TMDA katika kutekeleza sera ya viwanda, Kaimu Mkurugenzi wa Dawa na Vifaa Tiba, Akida Khea, alisema wawekezaji wa ndani wamepata mwamko mkubwa katika uagizaji dawa.

"Kati ya wawekezaji 16 waliokuja kuomba kujenga viwanda vya dawa na vifaa tiba, ambaye si Mtanzania ni mmoja. Maana yake wawekezaji 15 ni Watanzania. Hii itatusaidia kukuza kipato cha nchi na kuongeza ajira," alisema Khea.

Alisema wamehakikisha wawekezaji wanafuata taratibu zote za uanzishaji viwanda vya namna hiyo na wanawatembelea mara kwa mara ili kuhakikisha hawakiuki sheria.

# Silaha yatelekezwa ofisi ya serikali ya mtaa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

KATIKA hali isiyokuwa ya kawaida, silaha aina ya bastola imeokotwa ikiwa imetelekezwa na watu wasiojulikana nje ya Ofisi za Serikali ya Mtaa wa Maendeleo katika Kata ya Iyela, jijini Mbeya.

Jeshi la Polisi pia linamshikilia mzee mmoja Amani Mpendule (68), mkazi wa Kata ya Lualaje, wilayani Chunya kwa tuhuma za kukutwa na bunduki aina ya gobore iliyotengenezwa kienyeji bila kuwa na kibali.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema katika tukio la kwanza maofisa wa jeshi hilo waliiokota bastola hiyo aina ya Taurus ambayo imetengenezwa nchini Brazil.

Alisema bastola hiyo ina namba za usajili TGT.10582/PT 809 ambayo mmiliki wake hajafahamika na kwamba jeshi hilo linaendelea kufanya uchunguzi ili kubaini mmiliki wa silaha hiyo.

"Bastola hii iliokotwa Julai 25, mwaka huu, sasa unapokuta silaha kama hii katika mji huu ujuwe hata wahalifu wapo, hivyo tunaomba mtu yeyote ambaye anamfahamu mmiliki wa silaha hii atoe taarifa ili tuwakomeshe wahalifu hawa," alisema Kamanda Matei.

Katika tukio la pili, Kamanda Matei alisema Mpendule alikamatwa na gobore hilo ambalo analimiliki bila kuwa na kibali akiwa anaendelea kulitumia kwenye uwindaji haramu katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Alisema mzee huyo alikamatwa wakati wa msako wa pamoja kati ya maofisa wa Jeshi la Polisi na maofisa wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA) kwenye maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Chunya.

Alisema mbali na mtuhumiwa huyo kukamatwa na bunduki hiyo pia alikutwa akiwa na vipande vya nondo na baruti ambavyo alikuwa anavitumia kuua wanyama kwenye hifadhi hiyo.

"Tunaendelea kumhoji mtuhumiwa na ushahidi utakapokamilika tutamfikisha mahakamani kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria, hivyo natoa tahadhari kwa watu wote wanaomiliki silaha bila kuwa na vibali kuzisalimisha haraka katika Jeshi la Polisi," alisema Kamanda Matei.

Alisisitiza kuwa jeshi hilo litafanya msako wa nyumba kwa nyumba ili kuhakikisha watu wote wanaomiliki silaha bila kuwa na vibali wanakamatwa na kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria.



Wasukuma mkokoteni wakipita kwa tabu kwenye maji machafu yaliyotuama kwa muda mrefu katika Mtaa wa Kinazi, eneo la Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JULIANA OMARY-TUDARCO**

# Wafugaji wanufaika kiwanda cha maziwa

**Na Renatha Msungu, ARUSHA**

WAFUGAJI mkoani Arusha, wamenufaika na kujengwa kwa kiwanda cha maziwa cha Kilimanjaro Fresh baada ya kuwa na uhakika wa kuwa na eneo la kupeleka bidhaa zao za maziwa, ambazo awali zilikuwa zinaharibika.

Wamesema mikataba waliongia na kiwanda hicho imewasaidia kwa kiasi kikubwa kukuza kipato chao.

Teddy Sulle, mmoja wa wafugaji mkoani hapa, alisema Kilimanjaro Fresh imewasaidia kwa kiasi kikubwa kuinuka kiuchumi kwa kuwa sasa maziwa yao hayaharibiki tena kwa kukosa soko.

Alisema wanakishukuru kiwanda hiko na serikali kwa kuwa karibu na wenye viwanda ambao nao wanakuwa karibu na wafugaji.

Mkurugenzi wa Kilimanjaro Fresh, Irfhan Virjee, alisema kiwanda hiko kina mpango wa kuanza kupeleka maziwa Kenya ili kupanua soko la bidhaa zake.

Alisema lengo lao ni kuanza kuzalisha lita 30,000 kwa siku tofauti na sasa wanazalisha lita 10,000 kwa siku kutokana na ufinyu wa soko, akiongeza kuwa mkakati huo unalenga kuinua kipato cha wafugaji wa Mkoa wa Arusha na mikoa jirani.

"Tanzania ni wa pili kwa ufugaji wa ng'ombe barani Afrika. Kwa hiyo, tunapaswa kuwa juu hata katika uzalishaji wa maziwa," alisema Virjee.

Daktari wa Mifugo, Banson Ng'aida, alisema siri kubwa ya ng'ombe kutoa maziwa ni lishe bora na usafi kwa mifugo inayofugwa katika mazizi na wafugaji wengi wanakwama kupata maziwa mengi kutokana na kufeli katika eneo hilo.





Wafanyabiashara wadogo wakiendelea na shughuli zao, katika barabara ya CDA, jijini Dodoma jana. Halmashauri ya jiji hilo, imetenga eneo hilo kwa ajili ya wafanyabiashara hao ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa maeneo ya biashara. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# DC aonya udanganyifu wanufaika wa TASAF

**Na Paul Mabeja,** CHEMBA

MKUU wa Wilaya ya Chemba mkoani Dodoma, Simon Odunga, amewataka wawezeshaji watakaotumika katika halmashauri hiyo kufanya uhakiki wa kaya maskini zilizokuwamo kwenye kipindi cha kwanza cha mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), kuzingatia viapo vyao na kuacha kujihusisha na vitendo vya udanganyifu.

Odunga alitoa agizo hilo juzi alipofungua kikao kazi cha wakuu wa idara na mafunzo ya wawezeshaji wa halmashauri kuhusu utekelezaji wa kipindi cha pili cha mradi huo wa tatu wa TASAF pamoja na uhakiki wa kaya maskini.

Alisema wawezeshaji watakaohusika katika uhakiki wa kaya maskini, wanatakiwa kuzingatia viapo vyao ambavyo wataapa kabla ya kwenda katika maeneo ya utekelezaji.

Odunga alisema utaratibu wa kuwalisha viapo wawezeshaji hao utasaidia kuondoa udanganyifu kwa kuwa kwa atakayekwenda kinyume cha kanuni za utumishi wa umma, ataishia jela.

"Ndugu zangu wawezeshaji, tusifanye kazi hii kwa mazoea. Hivi viapo mtakavyoapa hapa, siyo kitu kidogo. Kwa yeyote ambaye atakwenda kinyume, basi itakuwa kazi rahisi kushitakiwa kwa mujibu wa viapo na sheria zilizopo," alionya.

Odunga pia aliwataka wawezeshaji hao kwenda kusimamia haki na kuacha kufanya udanganyifu katika uhakiki wa kaya maskini, akionya kuwa si sahihi kaya zisizo na vigezo kunufaika na mfuko huo kutokana na kupika taarifa za uongo.

"Sisi kama serikali hatuzivumilia kabisa kaya hizi hewa au zile zisizokuwa na sifa kuendelea kuwapo kwenye mpango huu wa kunusuru kaya maskini, hivyo basi mnapokwenda mhakikishe kuwa mnahakiki taarifa kwa umakini zaidi na sisi pia hata kwa gharama zetu tutahakikisha kuwa tunapita kujiridhisha," aliagiza.

Katika kikao hicho, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TASAF, ofisa kutoka makao makuu ya mfuko huo, Deo Shakiula, alisema mafunzo hayo ni ya siku tano.

Shakiula alisema siku mbili za kwanza watafanya mafunzo kwa nadharia na katika siku tatu za mwisho, watafanya kwa vitendo uhakiki katika kaya zilizoko kwenye mpango katika eneo husika.

"Mheshimiwa mkuu wa wilaya, mfumo huu ambao watautumia kufanya uhakiki wawezeshaji wetu, hauruhusu kabisa mtu kufanya udangajifu kwani watatumia vishikwambi ambavyo vitakuwa na uwezo wa kutoa taarifa ya eneo alipo na muda gani umetumika," alifafanua

Katika lengo la kufanya uhakiki wa kaya maskini ni kutekeleza agizo la Rais John Magufuli, alilolitoa wakati akizindua kipindi cha pili cha TAFAF Awamu ya Tatu, kiongozi huyo wa nchi akiagiza kufanyika uhakiki wa kaya maskini hewa zilizoko kwenye mpango.

Mratibu wa TASAF Wilaya ya Chemba, Simon Butondo, alisema jumla ya kaya 4,892 zilizokuwapo kwenye mpango huo katika kipindi cha kwanza na uhakiki utafanywa katika vijiji 42 ziliko kaya hizo kabla ya kuanza kwa utoaji wa ruzuku katika kipindi cha pili.

# Askari kampuni binafsi kupelekwa mafunzoni

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SHIRIKISHO la Wamiliki wa Kampuni za Ulinzi Binafsi (TSIA) Kanda ya Kati, limewataka wanachama wake kuhakikisha wanawapeleka kwenye mafunzo askari wao yanayotarajiwa kuanza mwezi huu.

Rai hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa shirikisho hilo, Kanda ya Kati, Lukanus Kayombo, alipozungumza na wandishi wa habari ofisini kwake jijini Dodoma jana.

Aliwataka wenye kampuni binafsi ya ulinzi Kanda ya Kati, kuhakikisha wanawapeleka askari wao kwenye mafunzo hasa wale ambao hawakupata mafunzo mwaka jana. "Ninawakumbusha wamiliki wenzangu wa kampuni za ulinzi nchini kuhakikisha tunawapeleka askari wetu kwenye mafunzo ambao hawajapata mafunzo na wanatakiwa kufanya hivyo Agosti mwaka huu. Kabla ya Desemba 30 tunatakiwa kufanya mafunzo hayo ili kutii agizo la Jeshi la Polisi ambao ndiyo wasimamizi wa kampuni zetu," aliagiza.

Alisema Kanda ya Kati wanategemea kuanza mafunzo ya kuwajengea uwezo askari mwezi huu ili kuhakikisha wanakamilisha kabla ya muda wa mwisho Desemba 30 mwaka huu uliowekwa na Jeshi la Polisi.

Kayombo, alisema kutokana na agizo la jeshi hilo, baada ya muda huo kupita askari ambaye hakushiriki mafunzo hayo ya miezi mitatu, hatakiwi kufanya kazi kwenye sekta ya kampuni ya ulinzi. Alibainisha kuwa, Kanda ya Kati yenye mikoa ya Dodoma, Manyara, Singida na Tabora, askari 550 walishiriki na kufuzu mafunzo hayo ya miezi mitatu yaliyoendeshwa na wakufunzi kutoka Jeshi la Polisi.

Aliitaja mikoa na idadi ya askari waliohitimu mafunzo hayo kuwa ni Manyara (100), Singida (100) na Dodoma (350) na hivyo kukamilisha idadi ya askari 550 waliopata mafunzo hayo kwa kanda nzima.

Kiongozi huyo pia aliwakumbusha wamiliki wa kampuni hizo kuhakikisha wafanyakazi wao wanakamilisha usajili kwa njia ya kieletroniki ili kuwatambua na kutekeleza agizo la Jeshi la Polisi linalowataka kukamilisha kabla ya Desema 30 mwaka huu.

Kayombo alisema kuweka majina hayo kwenye kanzidata kunasaidia kupata taarifa na mwenendo wa mfanyakazi husika kabla ya kumwajiri kwenye kampuni mpya.

"Kuna baadhi ya wafanyakazi wasio waaminifu, wamekuwa wakijihusisha na uhalifu mikoa mingine. Kama hakusajiliwa kwenye mfumo huo, anaweza kuajiriwa kumbe ni mwizi," alisema.

Aliongeza kuwa, faida ya mfumo huo wa kieletroniki ni kumwezesha kila mfanyakazi kuwa na taarifa zake ambazo zitamfanya afahamike kila eneo atakapokwenda kutafuta ajira.

# UWT wachekelea uamuzi wa NEC

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

JUMUIYA ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma, imefurahishwa na uamuzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kubadilisha majina ya majimbo ya Chilonwa na Mtera, ikisema inauunga mkono.

Majimbo hayo yaliyokuwa yanahudumiwa na jumuiya hiyo, yamebadilishwa majina, Chilonwa likiitwa Chamwino na Mterea likibadilishwa kuwa Mvumi.

Julai 23, mwaka huu, Rais John Magufuli wakati akizindua jengo la Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) wilayani Chamwino, alitoa ushauri jina la Jimbo la Chilonwa libadilishwe.

Siku chache baada ya Rais kutoa ushauri huo, NEC kupitia kwa Mwenyekiti wake, Jaji mstaafu Semistocles Kaijage, ilikubali ushauri huo na kutangaza majina mapya ya majimbo matatu nchini, yakiwamo hayo mawili.

Katibu wa UWT Wilaya ya Chamwino, Victoria Komba, alisema wamefurahishwa na uamuzi huo wa kubadilishwa majina ya majimbo hayo kwa kuwa hata wao yalikuwa yakiwachanganya.

Alisema kubadilishwa kwa majina hayo kutasaidia hata katika utendaji wao wa kazi kwa kuwa walikuwa wakikutana na wakati mgumu.


Katibu huyo pia alisema watiania 12 wa nafasi ya udiwani wa viti maalum katika majimbo ya Mvumi na Chamwino wamepitishwa kuomba ridhaa ya kugombea nafasi hiyo.

Alisema jumla ya wagombea 55 walijitokeza kuomba ridhaa ya kuteuliwa na CCM ambapo 12, walipitishwa na mkutano mkuu wa Jimbo wa Jumuiya ya Wanawake Wilaya ya Chamwino.

"Jumla ya wote walioijitokeza kuchukua fomu ni 57, ila mmoja hakurudisha na mmoja alijitoa, hivyo kufanya idadi ya waliochukua fomu kuwa 55," alifafanua.

Aliwataka walioongoza katika mchakato huo kutowadharau walioshindwa, akisisitiza kuwa hatua zingine bado zinaendelea ikiwamo kuwachuja wagombea, hivyo ni vyema wakashirikiana.

Pia, aliwataka kuondoa tofauti zao na kuhakikisha CCM inapata ushindi mkubwa kama ilivyoagizwa na Mwenyekiti wa Chama hicho Taifa, Rais Magufuli.



# Shein ataka vyama kunadi sera kwa amani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein, amevitaka vyama vya siasa kupitia wagombea wao kujinadi kwa wapigakura kwa kutangaza ilani na sera za vyama vyao na kuhubiri amani, umoja na mshikamano.

Akilihutubia jana Baraza la Iddi el-Hajj huko Bumbwini Wilaya Kaskazini B Unguja, alisema ni matarajio yake makubwa kuwa uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu, utakuwa huru na haki kutokana na kukamilika kwa maandalizi mengi mapema sana.

Hata hivyo, alisema uchaguzi huru na haki utatokana na wanasiasa wenyewe kujiepusha na kauli zenye lengo la kupandikiza chuki na uhasama.

"Huu ni mwaka wa uchaguzi ifikapo Octoba 28. Matarajio yangu makubwa ni kwamba vyama vya siasa kupitia wagombea wao vitajinadi kwa wapigakura kwa kutangaza ilani na sera huku msisitizo mkubwa ni kuhubiri amani na utulivu," alisema.

Dk. Shein aliwataka viongozi wa vyama vya siasa kutekeleza majukumu yao ya kufanya kampeni katika kipindi chote kwa kuzingatia sheria na kanuni za uchaguzi kupitia Tume ya uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

"Uchaguzi unaongozwa na sheria na kanuni ambazo viongozi wa vyama vya siasa vyote mnazijua kwa sababu mmefikia makubaliano na kusaini (kutia saini) matamko hayo... nataka myazingatie kwa makini sana," alisema.

Pia alisema kipindi cha harakati za kampeni za uchaguzi mkuu kitumiwe kama kipimo cha kutafuta viongozi, kisiwe cha kusababisha mifarakano na kupandikiza chuki za kisiasa. Dk.Shein alitumia nafasi hiyo kuwakumbusha Waislamu na waumini wengine kwa ujumla kwamba katika Kurani, Mwenyezi Mungu amewataka waja wake na kuwaambia washikamane na si kufarakana.

Kwa Dk. Shein, hiyo ilikuwa hotuba yake ya mwisho katika Baraza la Iddi kutokana na kumaliza muda wake wa kuwapo madarakani miaka 10 baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu.

Alisema sherehe hizo zimekuwa zikifanyika katika sehemu mbalimbali Unguja na Pemba ambazo zimekuwa zikitoa nafasi na fursa kwa Waislamu kujumuika na viongozi wao katika kufanya ibada.

"Sherehe hizi za baraza la Idd-el-Hajj ndizo za mwisho kwangu kufuatia (kutokana na) kumaliza muda wangu wa kuwapo madarakani. Ni utaratibu mzuri ambao umetuwezesha sisi Waislamu kujumuika pamoja na kubadilisha mawazo kwa ajili ya kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazotukabili," alisema.

Hata hivyo aliwapa pole Waislamu nchini ambao walikuwa katika matayarisho ya kuhuduria ibada ya Hijja huko Makka na kushindwa kutekeleza dhamira zao kutokana na janga la corona linazozikabili nchi mbalimbali duniani.

Alizitaka taasisi zinazoshughulikia safari ya ibada ya Hijja kufanya maandalizi ya mapema kwa mahujaji walioshindwa kufanya safari hiyo ili kutekeleza ibada hiyo kipindi kingine.

Dk. Shein alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kupambana na ugonjwa wa corona ambao kwa sasa umetokomezwa huku ikiwa hakuna hata mgonjwa mmoja katika vituo vilivyotengwa kulaza wagonjwa hao.

Aliwataka wananchi kuchukuwa tahadhari zaidi kwa sababu ugonjwa huo upo katika baadhi ya nchi jirani huku baadhi ya shughuli muhimu zikilazimika kusitishwa kutokana na tishio hilo.

Kadhalika, Aliwataka Waislamu hao kuwa na subra na uvumilivu kwani hiyo ndiyo mitihani ya Mwenyezi Mungu ambayo waja wake lazima kukabiliana nayo.

Naye Mufti wa Zanzibar, Sheikh Saleh Kabi, alimpongeza Dk Shein kwa uongozi wake bora katika kipindi cha miaka kumi ikiwa ni kigezo cha mfano wa kuiga.

Sherehe hizo zilihudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwamo Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Samia Suluhu Hassan, mgombea wa nafasi ya urais wa Zanzibar kwa tiketi ya CCM, Dk. Hussein Ali Mwinyi, na mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Muungano.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akisalimaina na Mama Fatma Karume, baada ya kumalizika kwa Baraza la Eid El Hajj, Wilayani Kaskazini (B), Mkoa wa Kaskazini Unguja. **PICHA: OMR**

# Chuo cha habari sasa sehemu ya SUZA

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHUO cha Uandishi wa Habari na Mawasiliano ya Umma cha Zanzibar (ZJMMC) kimekua sehemu ya Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kutokana na mabadiliko ya sheria nambari 11 ya mwaka yaliyopitishwa na Baraza la Wawakilishi.

Akikabidhi Chuo hicho kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Waziri wa Habari Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, alisema ni matarajio yake makubwa chuo hicho kitapata mafanikio kutokana na kuunganishwa na SUZA

Kombo alisema lengo la chuo hicho kupelekwa ni kuleta mabadiliko makubwa ya taaluma ya habari na kuleta ufanisi wa sayansi na teknolojia.

"Chuo cha uandishi wa habari cha Zanzibar sasa rasmi tunakikabidhi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ambacho kitakuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha taifa. Matarajio yangu ni kuwapo kwa mafanikio makubwa ya utendaji wake na kutoa wahitimu watakaokidhi vigezo," alisema.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Riziki Pembe Juma, aliwatoa hofu watendaji wote waliokuwa katika chuo hicho ambacho awali kilikuwa chini ya Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya kale kwamba haki zao zipo na zitaendelea kulindwa.

SUZA hivi sasa itakuwa na kampasi saba zikiwamo za Vuga, Benjamin Mkapa ilioko Pemba, Chuo cha Utalii kilichoko Chwaka, Chuo cha Kilimo cha Kizimbani na Chuo cha Ualimu cha Nkrumah.

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Dk. Idriss Muslim Hijja, alisema maandalizi yote ya chuo hicho kupelekwa SUZA yamekamilika ikiwamo maslahi ya watumishi wapya.

"Tulikuwa tukikamilisha baadhi ya mambo muhimu ikiwamo maslahi ya wafanyakazi wa chuo cha uandishi wa habari pamoja na mishahara na marupurupu yao na kuona hakuna malalamiko," alisema.

# SMZ sasa yafanya tathmini ya corona

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) imesema mchakato wa kufanya tathmini na kuhakiki taasisi na wajasiriamali ambao wameathirika na ugonjwa wa corona na kusababisha shughuli zao za kiuchumi kuyumba, unaendelea na upo katika hatua nzuri.

Waziri wa Fedha na Mipango, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa, alisema hayo wakati akitoa ufafanuzi kuhusu mchakato wa kufanya tathmini kuhusu athari za ugonjwa wa corona aliotangaza katika bajeti ya SMZ ya mwaka 2020/21.

Alisema ugonjwa wa corona umesababisha athari nyingi za kiuchumi kwa wajasiriamali na vijana ambao wengi wamerudi nyuma katika shughuli zao za maendeleo.

Ramia alisema licha ya serikali kufungua milango na kuruhusu kwa watalii kuingia nchini, bado hali haijawa nzuri kutokana na ukweli kwamba Ulaya bado ugonjwa huo unaendelea kuwa tishio.

Alisema serikali kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inaendelea na mchakato huo wa kufanya tathmini halisi za kiuchumi kwa makundi na wajasiriamali walioathirika na corona.

"Napenda kuwajulisha wananchi na makundi ya asasi za kiraia pamoja na wajasiriamali walioathirika na ugonjwa wa corona kutokana na miradi yao kuyumba kwamba Serikali inafanya tathmini kuhusu athari hizo na njia za kuwasaidia.

Baadhi ya wajasiriamali wamefurahishwa na juhudi hizo ambazo lengo lake kubwa kuwasaidia vijana na makundi mengine yaliyoathirika kiuchumi katika kipindi cha ugonjwa wa corona.

Zeyana Salum, mjasiriamali wa kijiji cha Bambi, alisema juhudi za makusudi zinahitajika kuchukuliwa ili kuyasaidia makundi mbalimbali, wakiwamo vijana na wanawake, yaliyoathirika kiuchumi kutokana na corona.



ZUCHU
UKURASA 12

JUMAMOSI AGOSTI 1, 2020



## SHILOLE NOMA!

# Kuwaacha wanaume si shida, Nuh na Uchebe yaleyale

MWANAMUZIKI na mjasiriamali, Shilole, ameweka rekodi ya aina yake kwa kuwaacha wapenzi wake Uchebe na Nuh Mziwanda, baada ya wote wawili kuachwa katika mtindo unaofanana.

Hivi karibuni, Shilole, alitangaza kumbwaga chini mume wake Uchebe, akitoa sababu za kuchoshwa na tabia yake ya ubabe pamoja na kupewa kipigo.

Hata hivyo, Shilole aliamua kucheza vizuri karata zake kwa kuwapa Watanzania mioyo ya huruma dhidi yake baada ya kusambaza picha zake tofauti zikimuonyesha akiwa na majeraha kutokana na kipigo.

Mtego huo umewafanya Watanzania na mashabiki wake, kuacha kufikiria jinsi msanii huyo aliyejaa vituko, huwa anawaacha vipi wapenzi wake.

Shilole huwa na tabia ya kuwaacha wapenzi wake na sio yeye kuachwa, kama alivyofanya kwa Nuh Mziwanda, aliyemuacha kwa visingizio kibao, ndivyo yalivyomkuta Uchebe, ambaye licha ya kunogeshwa asali tamu ya mapenzi, hatimaye alitupwa nje huku akimwagiwa shutuma kibao zinazompa taswira ya mwanamume mkatili.

Wote wawili, Nuh Mziwanda na Uchebe, wameachwa ghafla kiasi ambacho walijikuta wakichanganyikiwa na wote wanashindwa kueleza nini kimewatokea.

Licha ya kutunga wimbo wa 'Jike Shupa' kama kuondoa shinikizo la mapenzi, Nuh Mziwanda, amejikuta akitoa kauli za kumsihi Shilole, kufikiria mara mbili namna tabia yake ya kuishi na wanaume.

"Shilole kashakuwa mtu mzima aangalie cha kufanya maana kubadili wanaume ni kujitia aibu kila mtu ana upungufu, akae chini na mumewe wayaongee yaishe," amesema Nuh kwenye mahojiano yake ya hivi karibuni.

Hata hivyo, Uchebe yupo kimya akitafakari kwa kina kinachoendelea kati yake na Shilole, huku akionekana kutoamini kinachoendelea kwa sasa.

BASI SAWA

## Choki kupamba 'Kikao cha Wahenga' Morogoro

MWIMBAJI nyota wa muziki wa dansi, Ally Choki, anatarajia kushiriki uzinduzi wa albamu ya 'Kikao cha Wahenga' ya bendi ya Waluguru Original yenye maskani yake Morogoro.

Uzinduzi huo utafanyika mjini Morogoro, siku ya Ijumaa ijayo, huku ikipambwa na bendi ya The Bambazi, inayoongozwa na mwanamuziki wa zamani wa bendi ya FM Academia, Mulemule FBI.

Mkurugenzi wa bendi ya Waluguru Original, Killer Man, amesema amewaalika wanamuziki hao kwa kuwa ni miongoni mwa marafiki wa bendi yake hiyo.

Killer Man amezitaja nyimbo za albamu ya 'Kikao cha Wahenga' kuwa ni 'Morogoro Yetu, Mwanzo wa Mapenzi, Cha Kupewa, Ngalile Mwanangu Ndole, Supu na Nataka Nilewe'.

"Siku hiyo pia tutampigia Choki ataimba nyimbo zake, ila kwa upande wa Mulemule, atazimdua rasmi bendi yake yenye maskani jijini Dar es Salaam, lakini ameamua kuizindulia Morogoro," amesema Killer Man



## Rashida hukujua waswahili walivyo?

MWANAMITINDO, Rashida Wanjara, amekumbuka madhira aliyopitia kwa miaka mingi baada ya baadhi ya watu kumsema kuwa ni tasa kwa kukosa mtoto.

Rashida ambaye alikuwa Miss Mara, amefurahi kupata mtoto wake wa kwanza na kueleza uamuzi wa ujana ndiyo ulimchelewesha kupata mtoto.

"Wakati wa Mungu ni wakati sahihi, binafsi ujana na uamuzi ndiyo vilinichelewesha kupata mtoto, wapo watu walijua kuchelewa kwangu kuzaa kwamba nina matatizo maana nimeitwa Tasa nimeitwa Mgumba, kila mtu alikuwa ananijaji anavyojua yeye, ila mwisho wa siku ukweli nilikuwa naujua mimi mwenyewe" amesema wanjara.





## Ukimtaka Zuchu, fikiria mara mbili

WALE wanaotamani kumualika mwanamziki anayeng'ara katika muziki wa Bongo Fleva, Zuchu, sasa wanatakiwa kuvunja benki.

Meneja wa mwanamuziki huyo, Sallam_Sk, amesema kutokana na uwekezaji mkubwa walioufanya kwa msanii wao mpya, ni lazima mtu akusanye Sh. milioni 20 ndipo atampata.

"Gharama kubwa tumewekeza kwa Zuchu, ni lazima mtu atakaye mtaka alipe kiasi hicho cha pesa, vinginevyo hatuwezi kumruhusu," amesema Sallam.

## Mtoto wa Kununua: Mtoto si Mwanasesere

**Na Adam Fungamwango**

MWANAMUZIKI wa zamani George Mukabi aliimba wimbo wa 'Mtoto Si nguo', lakini Dk. Remmy Ongalla, naye akatunga wimbo akauita 'Nalilia Mtoto'. Wote walikuwa na maudhui yanayofanana kuwa binadamu anapokosa mtoto, inakuwa shida. Mtu anasononeka na hata kuvunjiwa heshima na jamii kwa kuitwa majina mabaya kama tasa na mgumba.

Wakati mwingine inasababisha kufanya jambo ambalo ni kinyume cha sheria ya kibinadamu. Mfano mzuri fuatilia filamu hii inayoitwa 'Mtoto wa Kununua'. Imechezwa na wasanii Mackie, Daim, Najma, Mastara, Savery, Suzy, Nyundo na wengineo.

Inaanzia mjini Tabora, mzee Nyundo anampokea mwanadada mmoja akitokea mkoani Arusha akiwa na kijana wake mwenye miaka inayozidi 18 anaiyeitwa Daim, waliokuwa wametoka huko akihangaika pa kuishi.

Siku ya kwanza Daim anakutana na kijana njiani anapewa pesa ambayo anadai analipa deni. Alichukua, lakini akashangaa. Siku ya pili Daim anapewa begi lenye mzigo ambao haujui anaambia tutakutana kijiweni. Anauchukua, lakini anashangaa pia.

Siku nyingine, Daim anakutana na wasichana watatu wanamsimamisha. Mmoja anawatambulisha kwa wenzake kuwa yule ni mpenzi wake. Daim anakataa kuwa yeye hana mpenzi. Msichana amuuliza yeye si Mackie?. Anajibu yeye ni Daim.

Upande wa pili wa shilingi kuna kijana anaitwa Mackie. Ni mmoja kati ya vijana wa kihuni mitaani.

Yeye ndiye aliyekuwa akiwadai pesa rafiki zake na mzigo. Anaanza kuwadai masela wenzake. Wao wanasema walishamlipa. Anashangaa. Mackie anakwenda kwa demu wake Leila. Kufika huko anafukuzwa kama mbwa na kuambiwa kuwa hawezi kuwa na mpenzi ambaye anamkana mbele ya rafiki zake. Mackie anashangaa tena.

Siku moja mama Daim na kijana wake wanapita njiani wanakutana na mtu akaanza kukimbia, mama anaanza kupatwa na




wasiwasi na kijana wake. Kwa nini akimbie? Akadani kuwa kijana wake amejiunga na makundi ya wahuni.

Mzee nyundo anamuona kijana wake anacheza pool, anaamua kwenda kumkataza, lakini akaambulia kipigo kwa vijana wale akiwemo kijana aliyedhania kuwa ni Daim.

Aliporudi nyumbani anasimulia yote kwa mama yake. Daim anaulizwa anashangaa na kukataa

Siku ya siku Mackie kalizua, kaiba mtaani. Wananchi wanamfukuza, lakini wakampoteza Mackie wanakutana na Daim njiani. Wakadhani ni yeye wakamkong'ota nusu ya kufa.

Masela wenzake wanamuokota na kumpeleka kwa mama yake. Bila kujua kuwa wamempeleka Daim kwa mama yake Mackie. Wakati anatibiwa majeraha, Mackie mwenyewe anaingia. Mshangao mkuu unawapata wote. Mama anaulizwa na kijana wake huyu ni nani na mbona kama wanafanana sana? Mama anaonekana kupigwa na butwaa bila majibu. Daim anaondoka.

Muda, Daim anarejea nyumbani kwa mama Mackie akiwa na mama yake. Kumbe wote wanajuana. Wanaitana majina. Najma ni mama yake Daim na Suzy mama yake Mackie. Ndipo kisa kizima kiliposimuliwa na fumbo kufumbuka

Kumbe miaka mingi iliyopita Najma alijifungua watoto mapacha. Aliyemsaidia kujifungua ndiye aliyemuibia mtoto, Najma akifahamu kuwa amejifungua mtoto mmoja tu, hivyo akaamua kuhama kutoka Arusha kwenda Tabora.

Alisema hakuna na uwezo wa kupata mtoto, hivyo alikashifiwa na wanaume na wanawake wenzake, hakuwa na amani ndiyo maana akafanya hivyo. Akamwambia wote wale ni watoto wake Najma, Daim akiwa ni Kurwa na Mackie ni Dotto.

Najma anamsamehe Suzy na kumkumbatia. Wakakumbatiana pia na watoto wao mapacha.





## Ferooz, Roma nao wamlilia Mkapa

WAKATI Taifa likiwa kwenye majonzi ya kuondokewa na aliyekuwa Rais wa awamu ya tatu Benjamin Mkapa, wasanii Ferooz na Roma Mkatoliki, wameomboleza kwa kutoa kibao cha kumuenzi.

Ngoma hiyo inaitwa Nalia, imetoka siku moja baada ya kiongozi hiyo kuzikwa kijini kwao Lupaso, mkoani Mtwara.

Ferooz ambaye alipewa zawadi ya gari na Mkapa baada ya kutoa ngoma yake inayoelimisha ugonjwa wa ukimwi, amesema atazidi kumkumbuka kutokana na kumpa moyo katika kazi yake ya usanii.

## WASANII WALIVYOMLILIA MKAPA

**Na Adam Fungamwango**

JUMATANO iliyopita, Taifa la Tanzania lilimpumzisha kaburini Rais wa awamu ya tatu, Benjamin William Mkapa, aliyefariki dunia usiku wa kuamkia Julai 24 jijini Dar es Salaam.

"Kwa masikitiko makubwa tumepata msiba mkubwa. Mzee wetu, Rais wa Awamu ya Tatu Benjamin Mkapa amefariki akiwa hospitalini mjini Dar es Salaam ambako alikuwa amelazwa," Ilikuwa ni sauti ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, akitangaza msiba huo."Tuendelee kumuombea Mzee Mkapa ambaye ametangulia mbele ya haki,"

Baada ya hapo, nchi iliingia kwenye kipindi cha siku saba za maombolezo. Kama kawaida nyimbo za maombolezo ndizo zilianza kushika chati kwenye vyombo mbalimbali vya habari, kama vile redio na televisheni.

Bendi mbalimbali za dansi, vikundi vya kwaya na wasanii mbalimbali, walianza kuingia studio, kufyatua nyimbo za maombolezo ambazo zilianza kupigwa kwa ajili ya maombolezo ya mzee Mkapa, aliyezikwa kwenye kijiji alichozaliwa cha Lupaso, Masasi mkoani Mtwara.

Hizi ni baadhi ya nyimbo zilizotolewa maalum kwa ajili ya msiba wa Mkapa na kutoa watu machozi.

**Pumzika Shujaa Mkapa-TOT Plus band**

Hili ni kundi la muziki linalomilikiwa na Chama Cha Mapinduzi, Tanzania One Thetre.

Kama kawaida yao tangu enzi la marahemu, Kapteni John Komba, muda mfupi tu walitoa kibao walichokiita' Pumzika Shujaa Mkapa'. 'Nenda Mkapa, umetimiza ile ahadi ulioahidi kwa Mola wako kuwa siku moja utarejea kwake, mbele yake nyuma yetu, nenda na ukalale salama." Ni baadhi ya maneno yaliyo kwenye wimbo huo.

**Kwa heri Mkapa-AIC Dar es Salaam Choir**

Kundi la kwaya ya Kanisa la Pentekoste Magomeni Mikumi jijini Dar es Salaam, maarufu kama AIC Dar es Salaam Choir, nao hawakuwa nyuma, kwani walikwenda studio haraka na kutoa kibao cha 'Kwa heri Mkapa' na kuwa mchango wao kuomboleza kifo cha kiongozi huyo na mwanadiplomasia mkubwa Afrika.

**Tutaonana Baadaye-Amos na Josh**

Wasanii hawa vijana wamebamba sana kwenye kipindi hiki cha maombolezo kwa ngoma yao ambayo inawaliza wengi. Wenyewe wanaiita 'Tutaonana Baadaye", na kuiimba kwa majonzi makubwa.

**Tundaman-RIP Mkapa**

Msanii Tundaman naye hakuwa nyumba, naye ameingia studio kutoa wimbo wa maombolezo, akiwa na baadhi ya wasanii wenzake, wakisema kuwa Mkapa ametutoka akiwa bado anahitajika.

**Asante Mkapa-Barnabasclassic**

Msanii wa siku nyingi, Barnaba, yeye kwa masikitiko makubwa alingoa studio na kurekodi kibao cha maombolezo ambacho jina lake ni 'Asante Mkapa.'

**Pumzika Salama-Beka Flavour**

Ngoma nyingine ya kumuomboleza Rais wa Awamu ya Tatu imetolewa na Beka Favour ambaye naye akaamua kutoa mchango wake kwenye nyanja ya sanaa kumuenzi kiongozi huyo kwa kutoa ngoma aliyoiita 'Pumzika Salama'.

**Pumzika Mkapa-Nasra Ft Pailot**

Kuna wimbo mmoja ambao huwatoa watu wengi machozi unaitwa 'Pumzika Mkapa'. Umetungwa na kuimbwa na wasanii wanaokuja juu, Nasra na Pailot.





# Kanye West ulitingisha kibiriti

MWANAMUZIKI maarufu wa marekani , Kanye West na mkewe, Kim Kardashian, hatimaye wameonekana pamoja kwa mara ya kwanza tangu kuibuka kwa taarifa ya wawili hao nusura watalakiane.

Kulingana na mtandao wa TMZ rapa huyo na mwanamitindo ambao ni mabilionea, walitoa picha ambazo wanaonekana wakiwa pamoja katika mahaba mazito.

Hivi karibuni, Kanye aliandika katika ukurasa wake wa twitter kwamba alifikiria kumpa talaka mke wake baada ya kumkuta akiwa na mwanamuziki mwenzake Meeck Mill.




## Duh! Fuse umechoma picha ya Yesu?

STAA wa muziki wa Ghana ambaye ana makazi yake Uingereza, Fuse ODG, ameibua mjadala mkali katika mitandao ya kijamii baada ya kuichoma moto picha ya Yesu.

Picha zenye uso wa mtu ambaye anaaminika kuwa ni Yesu kristo, imekuwa alama kuu kwa waumini wa dini hiyo na kitendo cha kuichoma moto inatafsiriwa kama uasi.

Kulingana na HYPERLINK "https://www.pulse.com.gh/entertainment/music/fan-injured-as-stage-collapses-at-fuse-odgs-kente-party/8k8m75j" \t "_blank" Fuse ODG, mchoro wa Yesu unaomuonyesha ana asili ya kizungu ni ubaguzi na ni sawa na kufananisha na dikteta au utawala wa kibaguzi uliokuwa Afrika Kusini.

## Tonto ukisikia ushujaa ndo huo

MWIGIZAJI kutoka Nigeria, Tonto Dikeh, ametoa kauli nzito ya kumsamehe aliyekuwa mume wake, Churchill Olakunle.

Tonto amesema kuna umuhimu wa kusamehe kwa watu walioumiza wenzao, hivyo naye ameamua kuweka wazi kwamba hana kinyongo na mumewe huyo walioachana.

"Kila siku naheshimu upendo, tuzungumze kuhusu kusamehe na nimekuja kueleza kwamba kusamehe si jambo la mtu mwingine bali linatoka kwangu," amesema Tonto.





## Joel pole kuondokewa na baba

MWIMBAJI kutoka Nigeria, Joel Amadi, maarufu kama Joeel, amesema baba yake ameuawa kwa kupigwa risasi na mtu asiyefahamika katika mji wa Kaduna.

Staa huyo aliweka ujumbe katika ukurasa wake wa Twitter, kwamba mtu mwenye silaha alimlenga baba yake na kumpiga risasi na kufa papo hapo.

"Ninajaribu kuwataarifu kwamba baba yangu mpendwa amefariki dunia kwa kupigwa risasi na mtu asiyejulikana. Mama na dada zangu wameshindwa kunijulisha kwa kunipigia simu kutokana na simanzi,"ametwiti

## Dr Dre, Nicole kugawana mali

RAPA mkongwe wa Marekani, Dr Dre, amejibu maombi ya talaka kutoka kwa mkewe Nicole Young, ikiwa dalili ya mwisho ya ndoa yao.

Kulingana na mtandao wa TMZ, mwanamuziki huyo maarufu duniani, amekubali kuweka saini makubaliano ya kuvunja ndoa pamoja na mgawanyo wa mali walizochuma.

Dre anaelezewa kuwa na utajiri wa dola milioni 800, na endapo mahakama ikisimamia mgawanyo huo, Nicole atajizolea mamilioni ya dola kama sehemu yake ya mali.



MAKALA

## YALIYOJIRI LIKIZO CORONA...

# Mwongozo mkoa wa 'Mwanga Elimu' ulivyolinda wanafunzi

## ■ Waliofikishwa wakiri 'tuko sawa'

**Na Happy Severine,** BARIADI

KABLA ya kuanza utekelezaji wa mpango mkakati wa kuwawezesha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari kusoma katika kipindi cha likizo ya dharura ya tahadhari ya ugonjwa wa Homa ya Mapafu (COVID 19).

"Nilipata wakati mgumu wa kufikiria ni namna gani nitaweza kuwasaidia wanafunzi wangu wa madarasa ya mtihani," ndivyo anavyoanza simulizi, Robert Mathias, Mkuu wa Shule ya Msingi Kidinda, katika Halmashauri ya Mji wa Bariadi, mkoani Simiyu.

Anasema baada ya kutangazwa likizo hiyo, alishikwa na mshituko wa ghafla uliomfanya ashindwe kufikiria cha kufanya kuwasaidia wanafunzi wake, aliyohitaji muda zaidi kuwanoa kitaaluma, kuwapa majaribio na maarifa ya namna ya kujibu vyema mitihani yao.

**UAMUZI GHAFLA**

Mathias anasema, kabla hajajua cha kufanya, alipokea taarifa zilizomtaka atekeleze mpango mkakati wa mkoa, wa kuwasaidia wanafunzi ndani ya likizo ya corona.

Ni agizo lililowangukia waliopo katika shule za msingi na sekondari, kwa kupatiwa majaribio na mitihani ya kuwapa maarifa katika masomo yao

Anasema, mara baada ya kupokea mkakati, ndipo alipoanza kuona mwanga na nuru ya mafanikio yake shuleni.

"Nilifurahi sana kupokea mkakati huo maana hapo nyuma kabla ya mlipuko wa ugonjwa wa corona shule yake ilijipanga kushika nafasi ya kwanza kimkoa, katika mitihani ya kitaifa. Hivyo, naamini kwa sasa mipango yetu itatimia," anasema.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mahaha, Charles William, akiwa ofisini kwake akieleza jambo kuhusu wanafunzi wake.

Pia, anaeleza kuwa wameutekeleza mkakati walivyoelekezwa, hata umeweza kuonyesha mafanikio makubwa, kutokana na wanafunzi kudumisha kumbukumbu za kutosha katika walivyojifunza.

Mathias anaueleza mkakati huo umewasaidia wanafunzi wake na shule nyingine ndani ya wilaya Bariadi, kupata masomo (vidokezo na majaribio)wakiwa nyumbani.

Ni kazi inayofanywa na walimu wao kupitia mkakati uliokuwa na malengo makuu manne yanayotarajiwa kuifanya Simiyu iendelee kufanya vizuri katika mitihani ya Taifa.

"Malengo makuu ya mkakati huo yalikuwa ni kumwezesha mwanafunzi kuendelea kujifunza, walimu kuwa na mawasiliano ya kitaaluma na wanafunzi wao," anaeleza Mathias na anaongeza:

"Wazazi kufanya kufuatilia taaluma za watoto wao pamoja na watoto (wanafunzi) kutulia nyumbani wakijisomea kipindi hicho cha likizo, huku tahadhari zote za maambukizi ya virusi vya corona zikizingatiwa."

Geodfrey Kamugisha, ni mwalimu wa taaluma shuleni hapo, anasema malengo yote manne yalifikiwa kwa mafanikio, hali inayowapa matumaini kuwa na utayari wa wanafunzi kufanya vizuri katika mitihani kitaifa wakiwa na ufaulu wa juu.

Anasema katika shule ya Kidinda, mpango umesaidia kuwafikia wazazi wa wanafunzi, wakiwapatia majaribio katika kipindi chote kilichopita cha tahadhari ya corona, wakiwa na mrejesho sahihi.

"Wakiwa nyumbani wanafunzi walikuwa wakijisomea na kufanya majaribio mengi zaidi. Wazazi walijitokeza kwa wingi kuja shuleni kuwachukulia majaribio na masahihisho yao.

"Pia, kwa mkakati huo imewasaidia sana wanafunzi kubaki na kumbukumbu ya masomo waliyofundishwa," anasema.

Anautaka kuwa ni mpango uliowezesha kuwasaidia wanafunzi wao wa madarasa ya mtihani, waendelee kujifunza na kusoma wakiwa majumbani.

Ni mazingira yaliyotumika kuchunguza kilichotumika kufanya mkakati na walibaini wanafunzi wengi kuwa na uelewa, pia kumbukumbu zinazopaswa kimasomo.

Kamugisha anasema, wanafunzi wote walio katika madarasa ya mitihani, walifanya majaribio mengi zaidi wakiwa majumbani na wote walirejesha majaribio hayo, ili wasahihishiwe na kupatiwa tena.

"Kwa wanafunzi wa darasa la nne, walifanya jumla ya maswali 2010, huku darasa la saba maswali 3500, ambayo yamewasaidia sana kutunza kumbukumbu na uelewa wao wakati wakiwa nyumbani," anasema Kamugisha.

Adalbert Chambia, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Gamondo, anaupongeza kwamba ni mkakati uliosaidia kudumisha njia sahihi ya kufanya vizuri katika mitihani kitaifa, chini ya kivuli cha mkakati wao mkuu kushika nafasi tatu za juu kitaifa.

"Bila ya kuwapo mkakati huo, sidhani kama wanafunzi wengi wangeendelea kuwa na kumbukumbu kama walizorudi nazo katika masomo yao," anasema.

**YALIVYOFAYIKA**

Mwalimu Mkuu huyo anasifu, majaribio yalikuwa yanatolewa kupitia shule, makanisa, misikitini na masoko makubwa, hali iliyowapa urahisi wazazi kufuatilia majaribio hayo.

Charles William, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mahaha, anakiri mafanikio ya kitaalamu kwenye likizo ya corona, asilimia kubwa ya wanafunzi waliyafanya kwa wakati na kupewa mrejesho.

Pia, anataja ushiriki wa wazazi kuwa wenye mafanikio makubwa, kwani wazazi walijitokeza kufuatilia mazoezi, jambo analoamini ni ishara sahihi kuelewa umuhimu wa ushiriki wao katika elimu ya watoto wao.

**WANAFUNZI WAELEZA**

Wanafunzi wa Shule za msingi Gamondo A, Kidinda na Mahaha, wanasema mpango mkakati wa kujifunza wakati wa likizo umewaongezea uelewa na ujuzi kujibu maswali, kutokana na kufanya mazoezi mengi kwa wakati.

"Tunawashukuru sana walimu na wazazi wetu...wamekuwa wakijitoa kwa kadri wawezavyo ili kuhakikisha wanatusaidia, tuweze kusoma wakati wa likizo.

"Wazazi wetu walikuwa wakitufuatia maswali shuleni," anatamka Maria Sayi, mwanafunzi darasa saba, shuleni Gamondo A.

Mwanafunzi Yohana Masunga, aliyeko darasa la nne, anakiri mpango kumsaidia kujifunza nyumbani na sasa anamudu majaribio mengi peke yake, kwa mbinu mbalimbali.

"Binafsi, mpango umenisaidia, wazazi walikuwa wakinifuatia maswali shuleni na nilifanya maswali yote na kupatiwa majibu na walimu.

"Kwa sasa sina shaka katika kujibu mtihani wa kitaifa, maana mbinu nyingi za kujibu maswali nimezipata vyema," Masunga

Wasi Boniphace, anayesoma mjini Bariadi, anadokeza hisia zake kwamba pasipo kutolewa mkakati wa kusoma likizoni, wanafunzi wa madarasa ya mitihani wangepoteza kumbukumbu ya walichokisoma kwa kiasi kikubwa.

Anaeleza nafsi yake wakati huo keamba hakupata shida aina yoyote kujisomea, kwani alisaidiwa mwongozo na mkakati uliowekwa na mkoa.



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mahaha, Charles William, akionyesha jarida lenye maelezo namna wanafunzi wanavyopaswa kujikinga na homa ya corona. **PICHA ZOTE: HAPPY SEVERINE.**



Rais mstaafu wa awamu ya tatu, Hayati Benjamin Mkapa (Kulia), akiwa na Hayati, Sir Andy Chande (katikati), kwenye moja ya matukio enzi hizo akiwa madarakani.

# Mkapa alikuwa rafiki mkubwa wa Sir Chande

**Na Joseph Mwendapole**

RAIS mstaafu wa awamu ya tatu, Hayati Benjamin Mkapa, ambaye alifariki Julai 23, mwaka huu alikuwa mtu aliyeijenga sekta binafsi ambayo aliamini kuwa ndiyo injini ya ukuaji wa uchumi.

Katika makala hii Mwandishi anaeleza namna Mkapa alivyopenda na kuwa karibu na mfanyabiashara mashuhuri ambaye sifa zake zilienea kitaifa na kimataifa tangu miaka ya 60 kutokana umahiri wake kwenye uendeshaji wa biashara zake na uongozi, Andy Chande.

Hayati Mkapa ambaye alizikwa kijijini kwake Lupaso Jumatano ya Julai 29 wiki hii, alipenda kuwa karibu na wafanyabiashara wakubwa, kuwapa moyo na kuwawekea mazingira bora ya kustawisha biashara zao akiamini kwamba sekta hiyo ni muhimili pacha kwa maendeleo ya uchumi.

Mmoja wa wafanyabiashara ambao Mkapa aliwapenda na kuwaona kwamba ni injini ya ukuaji wa uchumi alikuwa mtu kutoka Bukene mkoani Tabora, Sir Andy Chande mwenye asili ya Asia.

Chande ambaye kwa sasa naye ni marehemu amekuwa mfanyabiashara maarufu na mtumishi wa umma na alikuwa mfanyakazi asiyechoka katika vikundi vinavyotoa msaada hapa nchini na mataifa mbalimbali ulimwenguni.

Mkapa enzi za uhai wake akiwa madarakani na hata baada ya kustaafu, amekuwa mtu wa karibu wa Andy Chande, wamefanya mengi, wameshirikishana mengi kiasi cha Mkapa kuandika utangulizi kwenye Kitabu chake kinachoelezea maisha yake kitwacho Shujaa katika Afrika Safari kutoka Bukene.

Kwenye utangulizi wa kitabu hicho, Mkapa anamwelezea Sir Andy Chande kuwa mwanachama wa klabu ya Round table na Rotary aliyetunukiwa nishani ya ushujaa na dola ya kiingereza.

Alisimulia kuwa simulizi yake kwa Chande inajaribu kutoa picha ya maisha ya mtu na vile vile vituko vya wakati huo, yote mawili kwa ufasaha kabisa.

Kwenye andiko lake la utangulizi kwenye Kitabu hicho, Mkapa anasema mwanzo wa karne ya ishirini dunia ilishuhudia kuhamia Afrika Mashariki kwa wahindi waliokuwa raia wa Uingereza baadhi yao kusaidia ujenzi wa reli za Afrika Mashariki na wengine kujenga mtandao wa biashara eneo hilo.

Mkapa anasema mmoja wao, Keshavji Chande baada ya kujitumbukiza kwenye safari ya hatari ya meli kutafuta utajiri, alianzisha kitu ambacho wakati ule wa robo ya pili ya karne kilionekana chombo kikubwa sana cha biashara, kampuni iliyoitwa 'Chande Industries Limited'.

Anasema mwanawe Jayantilah Keshvji Chande maarufu kwa jina la mkato JK au Chande akiwa ndiye nguzo ya kampuni ile ya familia, ingawa kwa muda mfupi mno kutokana na kunaswa katika wimbi la kutaifishwa mali katika miaka ya '60'.

Mkapa anasema kwenye kitabu hicho, bila kukata tamaa aliendelea mpaka akawa mtu mashuhuri katika uendeshaji wa kampuni za viwanda na za biashara ambayo haikuwa yake tena bali sehemu ya kampuni ya biashara na viwanda yaliyomilikiwa na serikali ya Tanzania.

"Maelezo tunayoyaona humu kuhusu kipindi kile kabla ya Uhuru yamesheheni vituko, mivutano kati ya watu na matarajio ya mafanikio katika uchumi. Wazazi wa JK alikuwa wamebobea katika fani ya uhasibu, kukisia miradi inayoleta faida, kujitahidi kwa moyo wote kujenga uhusiano mwema na wakulima waliowauzia mazao na kununua mali iliyosindikwa au iliyoingizwa kutoka nje ya nchi," alisimulia Mkapa kwenye kitabu hicho.

Mkapa alisimulia kwenye utangulizi wa kitabu hicho kuwa ingawa hakuzipenda taratibu za elimu zilizokuwa na ubaguzi wa rangi, Chande aliitumia vema nafasi aliyopewa na familia iliyompenda sana, akitumia uzoefu wake akisaidia kuhakikisha kuwa mipango katika kipindi kile cha mpito iliwashirikisha watu wote na wa rangi zote.

Alisema miaka sita baada ya Uhuru wa Tanganyika ilikuja wimbi la kutaifishwa kwa shughuli muhimu za uchumi, shughuli zote za viwanda na biashara za familia ya Chande na za watu wengine zilitaifishwa na serikali.

"Ni uvumilivu na uzalendo wa mkubwa wa familia ya Chande, siyo tu kwamba walikiri hatua hiyo iliyochukuliwa na serikali lakini vile vile walikubali kwa moyo mmoja kusimamia mabadiliko ya kumiliki sehemu ya uchumi wa nchi. Kwa kuujua vema uwezo wa Chande katika biashara Rais Nyerere alimkabidhi kwa miaka mingi uenyekiti wa bodi za mashirika mengi ya umma," inasema sehemu ya andiko la Mpaka kwenye kitabu cha Andy Chande.

Kwenye kitabu hicho, Mkapa alisema kuwa Chande alikuwa mtu mwenye vipaji vingi, habari ya maisha yake haitakamilika bila kutaja mambo aliyoyapenda na kwamba mengi ya mambo hayo na madaraka aliyokuwa nayo yanashangaza kwelikweli.

Mkapa alifafanua kuwa alimfahamu Chande kwa mara ya kwanza kwa ari yake katika masuala ya elimu alipomweka kwenye bodi ya shule ya Shaaban Robert na baadaye akagundua kuwa alikuwa mtu mashuhuri kwenye shule ya viziwi kwani alikuwa mtu asiyepumzika kwenye shughuli za kusaidia jamii siyo kwa kuchangia tu bali kwa kuwahamasisha kwa moyo wake wote.

Alipozungumzia ndoa ya Chande na mke wake Jayli, Mkapa alisema Chande aliipenda sana familia yake na miaka 50 ya ndoa yake mapenzi yao yalianza kwa hofu lakini yakaishia kwenye pingu za uhusiano na mapenzi makubwa.

"Ukizungumza na mmoja wao utatambua jinsi alivyo na mapenzi makubwa mno kwa mwenzake, pamoja na mapenzi yao, wote wawili kwa watoto wao watatu wote wa kiume," inasema sehemu ya andiko la Mkapa kwenye utangulizi wa Kitabu cha Chande kilichoandikwa wakati huo wote wawili wakiwa hai.

Mkapa alisema Chande alitambuliwa na kupewa heshima na vyombo vya taifa na vya kimataifa heshima ambayo yeye Mkapa alisema Hayati Chande alistahili na kwamba anafurahi kuhusishwa na kutambuliwa kwa sifa na heshima anayopewa Chande kwani ni Mtanzania mashuhuri mwenye sifa za kimataifa.

Andy Chande alizaliwa Mombasa Kenya mwaka 1928 ingawa wazazi wake walikuwa wakiishi Bukene Tabora na alifariki dunia mwaka 2017 akiwa na miaka 89.

# Kenya yataja nchi zitakazoruhusiwa kutumia viwanja vyake vya ndege

**NAIROBI, Kenya**

KATIKA orodha ya nchi zitakazoruhusiwa ndege zake kutua Kenya, Tanzania na Burundi hazimo. Akizungumza jijini Nairobi, Waziri wa Usafirishaji, James Macharia, alisema kuwa anga la Kenya halitafunguliwa kwa kila nchi na nchi 11 pekee ndizo zitakazoruhusiwa raia wake kutua nchini humo. Macharia, alisema ni raia wa nchi hizo ambazo mbili kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na zilizobaki kutoka mataifa mengine, raia wake wataruhusiwa kutua katika viwanja vyake vinne vya kimataifa vya Nairobi, Mombasa, Eldoret na Kisumu.


Nchi zilizo ndani ya EAC zilizoruhusiwa ni Rwanda na Uganda, nchi zingine ni China, Korea Kusini, Japan, Canada, Zimbabwe, Ethiopia, Switzerland, Namibia na Morocco.

Waziri huyo, alisema nchi hizo zimedhibiti janga la Covid- 19 kwa kiasi cha kuridhisha.

Alisema nchi hizo zimepunguza maambukizi ya ugonjwa huo na raia wake wamekuwa wakipata dalili za kawaida za ugonjwa wa corona.

"Tutaendelea kuboresha orodha yetu kwa kutegemea na hali ilivyo na mazingira. Hii ni orodha yetu kwa leo tutaipitia tena kesho na siku zinazokuja." Alisema Alisisitiza "Abiria wote watakaowasili kwa ndege za kimataifa wakiwa na hati zinazoonesha kuwa hawana dalili za Covid-19 na wale waliopima saa 96 kabla ya safari hawatakaa karantini," alisema.

**BBC**



Waumini wa dini ya Kiislam, wakitekeleza ibada ya Hija kwa kuzunguka Kaaba, katika msikiti wa Maka huku akifuata kanuna za afya za jikinga na Covid-19 zilizotolewa na utawala wa Saud Arabia. **(AFP)**

# Waziri Mkuu Mali akataa kujiuzulu

**BAMAKO, Mali**

WAZIRI Mkuu wa Mali, Boubou Cissé, amekataa pendekezo la upinzani la kutaka ajiuzulu na kusema mzozo wa nchi hiyo utapatiwa ufumbuzi kupitia mazungumzo.

Akizungumza na Shirika la Utangazaji la Ujerumani (DW), Cissé alisema vuguvugu la maandamano nchini mwake linatakiwa kushiriki kwenye serikali ya muungano.

Madai ya upinzani ya kutaka kujiuzulu kwa Rais Ibrahim Keita na waziri mkuu wake, yamegonga mwamba kutokana na msimamo wa kiongozi huyo kuwa kujiuzulu kwao sio suluhisho la mzozo huo wa kisiasa.

"Kujiuzulu kwangu hakuko kwenye ajenda.Ni Rais pekee alie na mamlaka hayo, ya kuteuwa waziri mkuu na endapo haridhishwi basi anamtaka ajiuzulu.Tuna maelewano mazuri na Rais na mtizamo wetu wa pamoja wa kuwepo suluhisho la mzozo huu". Alisema.

Muungano wa kundi la vuguvu la M5-RFP, linaloandaa maandamano nchini Mali, umeitisha hatua nyingine za kuwataka wananchi kutotii sheria za nchi.

Kiongozi wa dini nchini humo, Ulamaa Mahmoud Dicko, mwenye ushawishi mkubwa kwenye vuguvugu hilo la maandamano, alisema kujiuzulu kwa waziri mkuu pekee hakuwezi kuutatua mkwamo wa kisiasa uliopo, bali kunaweza kuwa sehemu ya muafaka.

Aidha, alisema kuhusu pendekezo la viongozi wa jumuiya ya ECOWAS la kutaka kujiuzulu wabunge wanaolalamikiwa na wapinzani, alisisitiza hawatafanya hivyo kwa sababu ni kinyume na sheria za nchi hiyo.

Kwenye mkutano wa kilele kwa njia ya video kilichofanyika siku ya Jumatatu, viongozi wakuu wa nchi 15 za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Magharibi ya Afrika (ECOWAS) walisema wanamuunga mkono Rais Keita lakini wakatoa wito wa kuundwa kwa serikali ya pamoja.

**DW.**

# Marekani yaonya kuongeza muda vikwazo Iran

**WASHINGTON, Marekani**

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Mike Pompeo, ameonya nchi yake italazimisha kuongeza muda wa vikwazo vya Umoja wa Mataifa dhidi ya Iran, ikiwa muda wake utamalizika.

Hata hivyo, Urusi na China ambazo zina kura ya turufu kwenye Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, zinataka Iran iuziwe silaha za kawaida baada ya muda huo kumalizika mwezi Oktoba.

Vikwazo hivyo viliwekwa kwa mujibu wa azimio la Umoja wa Mataifa la mwaka wa 2015. Waziri Pompeo aliaambia kamati ya mambo ya nje ya baraza la seneti la Marekani, kwamba nchi hiyo itapendekeza azimio hilo kurefusha muda.

Waziri huyo alieleza ikiwa azimio hilo halitapitishwa, Marekani itachukua hatua za lazima kuhakikisha Iran, inaendelea kuwekewa vikwazo.

Hata hivyo wanachama wengine wa kudumu kwenye Baraza la Usalama, Uingereza na Ufaransa walisema suala la kipaumbele ni kutafuta suluhisho la kidiplomasia ili kukomesha mpango wa nyuklia wa Iran.

**DW**

# Ulaya yaiwekea vikwazo China, Urusi

**BERLIN, Ujerumani**

UMOJA wa Ulaya umeziwekea China, Urusi na Korea Kaskazini vikwazo kwa kuwapiga marufuku maofisa wa idara za ujasusi za nchi hizo kuingia katika nchi za Umoja wa Ulaya.

Hatua hiyo inatokana na madai ya idara hizo kushiriki katika shughuli za udukuzi wa kimtandao duniani kote.

Idara hizo za ujasusi zinatuhumiwa kujaribu kufanya udukuzi kwenye shirika la kudhibiti silaha za nyuklia.

Waliowekewa vikwazo hiyvo ni maofisa sita na taasisi kadhaa za nchi hizo tatu.

Katika kujihami dhidi ya hujuma za kimtandao, umoja huo ulipitisha utaratibu wa kisheria wa kuuwezesha kuweka vikwazo kwa mataifa adui. Vikwazo hivyo pia vitahusu kuzuia mali za watu na taasisi husika.

**DW.**

# HADITHI

# Mauaji Harusini-23

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awe navyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele.

Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**

"Kwa muda mrefu nimekuwa kama sina furaha hivi kwenye maisha yangu na hasa baada ya mama kufariki nikiwa bado mdogo, nimeishi kwenye familia ya kitajiri nikipata kila kitu, lakini faraja na amani ya moyo nilikuwa sina hadi nilipokutana na wewe siku ile."

"Shani ni kitu gani ambacho wewe unadhani mimi ninacho kilichokufanya sasa uwe na furaha na amani?" Eddy alizidi kumchimba mwenzake.

"Sijui, basi tu. Tangu siku ile makaburini tulipokutana, ulipoondoka na mimi kuondoka, niliona kabisa kama moyo wangu umekuwa unahitaji kukufahamu zaidi na hata ulipoanza kuwa unanisalimia na kuwasiliana na mimi, kusema kweli moyo wangu ulionyesha unakuhitaji sana."

Eddy alitazama Shani kwa makini na kugundua kuwa anachokisema kilitoka rohoni na si mdomoni.

"Leo nitapenda kukwambia kitu kimoja tu. Shani nakupenda sana zaidi ya neno lenyewe na naahidi nitaendelea kukupenda na kukujali siku zote. Na hii siyo kwa sababu wewe unasema umekuwa na faraja na amani ya moyo kuwa na mimi, ila nilipokuona kwa mara ya kwanza tu kule makaburini moyo yangu ulikuwa tayari umeshawaka juu yako, naahidi nitakupenda na sitokuangusha au kukukwaza."

Taratibu machozi yalianza kumtoka Shani. Alijisogeza karibu na Eddy akamkumbatia. Akajilaza kifuani.

"Usinione hivi Eddy, mimi nimekuwa na matatizo makubwa. Na hadi leo bado nina matatizo makubwa. Na sikuwa na mtu yoyote wa kushea naye matatizo yangu. Wewe ni rafiki yangu, naomba tuwe pamoja kwenye furaha na matatizo yangu." alilia Shani.

"Najua. Najua Shani. Tutakuwa wote. Sitokuacha peke yako. Ila kuna siku ningependa uniambie matatizo yote yaliyokupata huko nyuma, yaliyokuwepo na ambayo unaona kama yatakuwa kikwazo kwako."

"Nitakwambia, lakini siyo hapa. Nitakwambia sehemu maalum. Tukiwa wawili tu.

***************************************

Ilikuwa ni kama sinema au tamthilia tamu iliyopita jana. Akiwa kitandani alikuwa akirudia kukumbuka yale yote aliyoyotokea jana kwenye hoteli ya ABC Club. Ilikuwa ni saa 12 asubuhi alipoamshwa na kengele ya saa. Tayari usingizi ulikuwa umemtoka. Alikuwa anataka kutoka kitandani na kujiandaa kwenda kazini.




Lakini akili yake ilirejea alipokuwa na mrembo Shani. Kwa hakika jana ndipo alipomfahamu kinagaubaga msichana huyo.

Alichogundua ni kwamba Shani ni msichana aliyeachiwa utajiri mkubwa na baba yake Patiyo, lakini pamoja usomi wake anahitaji msaada mkubwa ili aendelee kuushikilia na kuuendesha.

Si kwa sababu yeye ni mtoto wa kike tu, umri pia bado mdogo, lakini vilevile anahitaji watu na wasimamizi sahihi wa kumsaidia.

Akumbuka jinsi mtoto wa kike alipomlilia machozi mara mbili. Mara ya kwanza ni pale alipokuwa akimwambia anamhitaji, lakini mara ya pili ni pale walipoachana kila mmoja akirejea kwake.

Alimkumbatia na kumwambia maneno ambayo bado yamekuwa yakijirudiarudia kwenye ubongo wa Eddy.

"Hata kama nakosea, lakini ukweli lazima niseme tangu nianze kukuona wewe kwa mara ya kwanza na kuanza mawasiliano na kukutana, wewe umekuwa unanipa faraja na amani, sikufikiria kama nitakuwa na furaha kama hivi sasa tena maishani mwangu. Naomba usiniache, sitaki kukupoteza Eddy."

Kama mwanaume yoyote yule mwenye jukumu la kumpa faraja mwanamke na kumbembeleza, Eddy alimpapasa kichwani kwenye nywele zake ndefu hadi mgongoni.

"Usijali mama tutakuwa pamoja kwa shida na raha. Tutaambatana na kubembelezana kama vipepeo wawili wapendanao."

Shani akimtazama Eddy akapeleka mdomo wake kwenye shavu akambusu. Eddy naye alijibu kwa busu matata. Wakaagana. Lakini kila mtu alikuwa bado ana hamu na mwenzake. Hakuna yoyote aliyetaka kufanya haraka.

Wakati Shani akiwa amezama kwenye penzi la Eddy, kwa upande wake Eddy pamoja na kuzama kwenye mapenzi, bado akili yake ilifanya kazi haraka sana. Akili ni ile ile ya kipelelezi. Alikuwa kwenye mapenzi, lakini hapo hapo alikuwa makini kwa kila kitu.

Na ndiyo maana hakwenda kizembe. Alifika saa moja kabla ya Shani kufika. Kosa moja alilotaka kufanya ni kukataza chakula kisiletwe baada ya kuokota kifuko cha sumu kutoka kwa mmoja wa wahudumu wa kiume.

Akili yake iliendelea kufanya kazi haraka na papo hapo akabadilisha maamuzi na kumtaka mhudumu yule amletee Shani chakula. Alijua Shani pale ni mteja wao, hivyo hakutaka kuweka kitu kama uhasama, lakini pia kumshtua mhudumu yule na Shani. Wote wangehisi kuna kitu ambacho si cha kawaida. Hili Eddy hakulipenda, ndiyo maana akabadilisha kauli. Lakini pia alikuwa na lingine moyoni.

Alipomruhusu mhudumu yule amletee Shani chakula, alikwenda moja kwa moja kama anaelekea msalani na kukutana na mhudumu wa kike, akamsimamishwa na kumuuliza swali.

"Dada, yule msichana unamfahamu?"

"Ndiyo ni mteja wetu huwa anakuja mara kwa mara kupata chakula cha mchana."

"Namtaka yule msichana anafaa?"

Swahi hilo lilimfanya mhudumu yule kuangua kicheko.

"Si ulikaa naye pale wewe mimi nakuona, halafu unaniuliza mimi tena."

"Basi anafaa, sasa mimi nataka 'nimsapraizi', huwa anapenda chakula gani yule?"

"Anapenda sana biriani yule dada, ndiyo huwa anakuja kula kila Jumamosi hapa."

"Basi tuletee mbili mimi na yeye."

Eddy alikumbuka maneno aliyoongea na msichana yule aliyekutana naye wakati akijifanya kuelekea msalani, akaongea naye kwa sekunde kadhaa, kabla ya kuelekea msalani kupoteza lengo, haraka, akarejea kumuwahi Shani asile kile chakula ambacho alikuwa na wasiwasi nacho, baada ya awali kuokota kifuko cha sumu, kilichoanguka kutoka kwa mhudumu yule wa kiume wa hoteli hiyo ya ABC Club.

Akiwa kitandani, Eddy alikumbuka jinsi alivyotoka tena kuelekea msalani, akampa ishara mhudumu yule yule wa kike amfuate na kumpa maelekezo kadhaa.

"Unakiona kile chakula kilichopo pembeni?"

"Ndiyo."

"Shika hii." Eddy alimkabidhi mhudumu yule kibunda cha noti mpya shilingi laki moja.

Ingawa mhudumu yule hakujua idadi kamili ya pesa zile, lakini alijua ni pesa za kutoka, lakini alizipokea akiwa na mshangao.

"Ananitaka?" Aliwaza. "Lakini huyu si ana yule msichana pale?" Mawazo yalizidi kumvuruga mhudumu yule.

"Usijali dada mzuri, unaitwa nani?"

"Diana."

"Okay, Diana, naomba unifanyie kazi moja tu, lakini iwe siri yangu mimi na wewe, usimwambie mtu."

Diana alibaki amepigwa na butwaa asijue akatae au akubali, bila hata kujua ni kazi gani anayotaka kuambiwa.

"Ni hivi, nataka uje uchukue kile chakula kilichopo pembeni yetu, alicholeta yule mhudumu mwenzako wa kiume. Ukichukue, lakini usiende kukimwaga, ukiweke sehemu yoyote ile nzuri, ukihifandhi kwa sababu mimi nataka kukichukua." Eddy alimwambia Diana.

Bado kwenye uso wa mhudumu huyo ulionekana kama kuna maswali mengi ya aliyokuwa anajiuliza.

"Diana, tafuta mfuko, kimwage chakula hili kwenye mfuko, halafu kama unaweza kutoka nacho, leo, kesho au kesho kutwa tuwasiliane, halafu unikabidhi, nakihitaji."

Mshangao wa Diana ulikuwa ni kwa nini mwanaume yule anakitaka kile chakula ambacho hakikuliwa na yeye au mpenzi wake. "Je anataka kumpeleke mbwa?" Alijiuliza.

"Lakini kwa nini aseme asijue mtu? Kwani kama ni kumpelekea mbwa si angemwambia tu akakikuchukue, akatafute mfuko akifunge na kumpelekea, badala yake anataka iwe siri?" Bado Diana alijiuliza.

Lakini kwa sababu tayari alikuwa na pesa mkononi. Na pia kwake haikuwa kazi kubwa sana. Ni kukichukua tu, kwenda jikoni kutafuta mfuko madhubuti na kukitia humo, baadaye kutoka nacho, basi alikubali.

Haraka, Walibadilshana namba za simu na kazi ikawa imekamilika.

Siku hiyo Eddy alitarajia kutaka kumpigia simu Diana ili wakutane sehemu akichukue chakula hicho.

Lengo ni kukipeleka kwa mkemia mkuu ili kujua kama kina dalili yoyote ya sumu. Na kama sumu ni ya aina gani? Kama haina basi wasiwasi wake utakuwa ni wa bure. Lakini kama kuna sumu ndani ya chakula. Na yeye aliokota kifuko cha sumu kilichoangushwa na mhudumu aliyemletea Shani chakula, basi tatizo litaanzia hapo.

*Itaendelea Jumamosi*

MAKALA MAALUM

# Bilioni 23/- zinavyoisuka upya Kariakoo

## ■ Uongozi mpya waipa mamilioni TRA
## ■ Kariakoo nyingine kujengwa Tabata

Na Enock Charles

UNAPOTAJA Kariakoo kwa Kiswahili cha mitaani 'ni jina kubwa mjini'. Hicho ni kitovu cha Jiji la Dar es Salaam ambacho kimeteka biashara siyo tu kitaifa, bali Afrika Mashariki na Kati.

Hapo unataja wateja wa bidhaa zaidi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), kwa uchache unawataja watu kutoka Malawi, Zimbambwe, Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Umaarufu wa Kariakoo kibiashara si wa jana wala juzi, bali unaenda sambamba au hata zaidi ya uhuru wa nchi uliopatikana miaka zaidi ya 50 iliyopita.

Hilo ndilo chimbuko la aliyekuwa Rais wakati huyo, Hayati Mwalimu Julius Nyerere kuchukua hatua za makusudi katikati ya Kariakoo yenyewe, akaipa kandarasi Kampuni ya Ujenzi ya Mwananchi (MECCO) kujenga soko la kisasa ambalo kwa wakati huo halikuwa na mpinzani.

Jengo la aina yake ambalo halina kingo za kawaida zilizozoeleka katika majengo yaliyotapakaa kila mahali, chini yake kukiwa na eneo lililobuniwa, maarufu kwa jina la 'shimoni' ambako ndiko kulikuwa soko kuu la jumla.

Mfumo mzima wa soko hilo linalopambwa na masoko madogo nje yake, Desemba 8, 1974 baada ya kukamilika, serikali ililiundia taasisi inayodumu hadi leo inayoitwa Shirika la Masoko Kariakoo (SMK).

Meneja Mkuu wa Shirika hilo, anasema limeendelea kujidhatiti kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwa ni moja ya jitihada zake za kuwekeza zaidi kibiashara.

Hetson Msalale anasema katika uongozi huu wa serikali, shirika limefanya mageuzi makubwa ambayo mbali na kuongeza wigo wa mapato, pia limeboresha huduma kwa wananchi.

Anabainisha kuwa shirika limekuwa katika mpango mkakati wa kutekeleza miradi mikubwa ikiwamo kuboresha jengo la soko dogo kwa kujenga jengo la kibiashara kubwa na la kisasa. Anasema mradi huo unakadiriwa kugharimu Sh. bilioni 23.

"Haya ni mafanikio makubwa kwetu, kwani tumepanua huduma zetu ili wateja wetu wafanye biashara zao katika mazingira bora zaidi," anasema.

Msalale anasema shirika pia liko katika hatua ya kutekeleza miradi mingine mikubwa ukiwamo wa ujenzi wa soko lingine katika viwanja vyake vilivyoko eneo la Mbezi Beach Makonde katika Manispaa ya Kinondoni.

Msalale anasema kuwa mradi huu pia unakadiriwa kuwa na thamani ya zaidi ya Sh. milioni 500 hadi kukamilika kwake huku wakijipanga kuwekeza katika miradi mingine ya aina hiyo kwenye viwanja vyao vilivyoko Tabata Bima katika Manispaa ya Ilala.




Judith Magoto, mkazi wa Jiji la Dar es Salaam, analishauri Shirika la Masoko Kariakoo kuendelea kuboresha huduma zake, akisema: "Waboreshe usafi katika soko, hayo ndiyo mambo tunayoyataka wateja wa soko hili."

Mzee Ali Shija, mfanyabiashara wa Kariakoo kwa muda mrefu, anaungana na Magoto kulipongeza soko hilo kwa kuboresha mazingira .

"Kwa sasa hali ya usafi na usalama imeimarika sana na tunaweza kufanya kazi zetu kwa usalama zaidi," anasifu na kuushauri uongozi wa shirika kuwekeza katika maeneo mengine kandokando ya jiji, ili kusogeza huduma zake karibu na wananchi.

**MAFANIKIO**

Msalale anabainisha kuwa katika kipindi cha miaka mitano ya uongozi wa sasa wa serikali, shirika hilo limefanikiwa kuongeza mapato yake kutoka Sh. bilioni 2.115 mwaka 2015/16 hadi kufikia Sh. bilioni 3.351 mwaka 2019/20, sawa na ongezeko la asilimia 63.1.

Anasema kupaa huko kwa mapato kumetokana na kuongeza kwa ufanisi katika usimamizi matumizi ya mfumo ya kielektroniki wa kukusanya mapato ya serikali (LGRCIS na udhibiti wa mianya ya upotevu wa mapato ya shirika.

Msalale anabainisha mafanikio mengine kuwa ni kuimarika kwa usafi wa soko hususani katika uondoshaji taka na mazingira kwa ujumla, hivyo kudhibiti magonjwa ya mlipuko na kuepusha athari nyingine zinazotokana na uchafu.

Anasema mifumo ya hewa katika eneo la shimoni imeboreshwa na kufanyiwa ukarabati wa mara kwa mara, hivyo kuweka mazingira rafiki kwa wafanyabiashara kwenye eneo hilo.

"Shirika limegharamia na kufunga mfumo wa kamera za CCTV kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama wa soko, ili wafanyabiashara na mali zao pamoja na wateja wanaotembelea soko wawe salama," anasema.

Anayataja mafanikio mengine kuwa ni uboreshaji wa maeneo ya kufanyia biashara kwa lengo la kuongeza mapato ya shirika kwa kujenga miundombinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na maduka 94 kuzunguka jengo la Soko Kuu, ujenzi wa paa katika eneo la soko la wazi na ujenzi wa maduka 19 katika Mtaa wa Tandamti.

Anasema kuwa idadi ya maduka imeongezeka katika kipindi hicho cha miaka mitano, kukiwa na maduka 113 yaliyowezesha kuongezeka kwa mapato kwa wastani wa Sh. miloni 56. 5 kwa mwezi, sawa na Sh. milioni 678 kwa mwaka.

Mafanikio mengine ni kugharamia maandalizi kuelekea biashara ya saa 24 katika eneo la Kariakoo, ambapo maeneo mbalimbali kuzunguka soko yamefungwa taa na kamera 24 za CCTV kwa lengo la kuimarisha ulinzi na usalama.

"Shirika limefanikiwa kuboresha mazingira ya watumishi kufanya kazi kwa kuongeza vitendea kazi kama vile kompyuta na samani za maofisini pamoja na kununua gari jipya la shirika.

"Pia, tumefanikiwa kulipa mchango kwa serikali kuu ambapo katika mwaka wa fedha 2018/2019, shirika limelipa Sh. milioni 50. Shirika limefanikiwa pia kuandaa rasimu ya marekebisho ya sheria ya shirika, ili kuendana na wakati uliopo ambapo wanahisa wote wawili (Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Msajili wa Hazina) wamekwisha toa maoni yao.

"Hatua inayofuata ni ya kukusanya maoni ya wadau wengine ili kukamilisha rasimu na kuiwasilisha Ofisi ya Rais -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI)," anabainisha.

Meneja Mkuu huyo pia anasema wamefanikiwa kuhuisha mipaka ya maeneo yanayomilikiwa na shirika kupitia Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, ili kuhakikisha maeneo hayo yanalindwa kwa maslahi ya shirika na kuepuka uvamizi.

Anasema wamefanikiwa kurejesha kwenye umiliki wa shirika jengo la ghorofa lililoko eneo la Tabata Bima ambalo lilikuwa limeuzwa kwa njia ya mnada wa mahakama.

Vilevile, anasema shirika limefanikiwa pia kurejesha eneo lake lililovamiwa la Mbezi Beach Makonde lenye ukubwa wa mita za mraba 6,119.

Anasema katika kipindi hicho cha miaka mitano, shirika limefanikiwa kutoa ajira kwa watumishi na wataalamu wapya 45. Kati yao, 29 ni waajiriwa wa kudumu na 16 ni watumishi wa mkataba.

Msalale anabainisha kuwa ni katika uongozi wa sasa wa serikali, shirika limepata uongozi kamili kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Namba 36 ya mwaka 1974 iliyolianzisha.

Anafafanua kuwa Rais Magufuli, kwa mamlaka aliyonayo kikatiba, amewezesha kuundwa kwa Bodi ya Wakurugenzi kwa kumteua Mwenyekiti wa Bodi na pia kumteua Mtendaji Mkuu wa Shirika ambaye ni Meneja Mkuu.

"Ni muhimu kufahamu kwamba, Shirika la Masoko ya Kariakoo kuanzia mwaka 1999 hadi Desemba 2015, lilikuwa halina uongozi na utawala unaoelekezwa katika sheria yake iliyoanzisha shirika.

"Kwa hiyo, kutokana na hali hiyo, shirika lilikosa uongozi kwa mujibu wa sheria. Matokeo yake, hali hiyo ilikuwa na madhara kwa shirika ikiwa ni pamoja na kuyumba kiutendaji na kukwama kwa miradi mbalimbali ya kimaendeleo," anasema.

Anabainisha kuwa, katika kipindi hicho cha miaka 16 ya kukosekana kwa uongozi sahihi, shirika liliingia katika madeni makubwa yakiwamo ya PAYEE, SDL na Kodi ya Ardhi kwa serikali, yaliyokuwa yanafikia Sh. bilioni 1.3.

Msalale anasema kuwa, shirika katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, limefanikiwa kuongeza bajeti kwa asilimia 32.4 kutoka Sh. bilioni 2.5 kwa mwaka (mwaka wa 2015/2016) hadi kufikia bilioni 3.7 mwaka 2019/20.

"Kama ilivyotangulia kudokezwa katika sehemu ya kwanza ya mafanikio kwamba shirika limepata uongozi wenye kutambuliwa kisheria, tumefanikiwa kupunguza deni la Sh. bilioni 1.3 lililokuwapo," anasema.

Anafafanua kuwa, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2016/17 hadi 2019/20, shirika limefanikiwa kulipa madeni mbalimbali kwa serikali yenye jumla ya Sh. milioni 800 kati ya Sh. bilioni 1.3 ambazo lilikuwa linadaiwa.

Sambamba na kulipa kiasi hicho cha deni la nyuma, Msalale anasema shirika sasa linawasilisha makato yote stahiki ya kisheria kila mwezi katika mamlaka husika ikiwamo PAYEE katika mamlaka ya Mapato (TRA).

"Haya ni mafanikio makubwa ndani ya shirika chini ya uongozi wa Rais John Pombe Joseph Magufuli tangu alipoingia madarakani na kuamua kuweka uongozi madhubuti katika shirika kama sheria ya shirika inavyobainisha katika muundo wake," anasema.

Shirika la Masoko ya Kariakoo lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 36 ya Mwaka 1974 ili kusimamia eneo hilo la kibiashara ambalo limesheneni aina mbalimbali ya bidhaa ambazo pia husafirishwa na kuingizwa sokoni kutoka maeneo mbalimbali ya nchi na hata nchi jirani kama vile Zambia na Malawi ambako baadhi ya mazao yanayozalishwa katika nchi hizo huingizwa katika soko hilo.

Msalale anasema shirika limepita katika vipindi mbalimbali vya kimaendeleo ambavyo pia vilikumbana na vikwazo kadhaa katika miaka hiyo miaka 45 tangu kuanzishwa kwake.

# RUMMENIGGE ATHIBITISHA THIAGO KUONDOKA BAYERN

**MUNICH, Ujerumani**

KOCHA wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge amethibitisha kwamba, Thiago Alcantara anayewaniwa na Liverpool ataondoka kwa mabingwa hao wa Bundesliga.

Thiago mkataba wake unamalizika mwakani hapo Bayern na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, raia wa Hispania ameripotiwa kwamba yupo tayari kuondoka kwa 'Bavaria' hao baada ya kukataa kuongeza mkataba mpya.

Jurgen Klopp inaaminika kwamba anamuwania Thiago atu pale Anfield, ambapo Liverpool walishinda taji lao la kwanza la Ligi Kuu tangu 1990 msimu huu.

Wakati uvumi ukitawala kuhusu majaliwa ya Thiago, Rummenigge amesema kiungo huyo wa zamani wa Barcelona yupo tayari kwa changamoto mpya.

"Kwa uhakika majalidiliano na (mkurugenzi wa michezo), Hasan (Salihamidzic) aliyofanya naye yalikuwa na mafanikio makubwa.

"Thiago alimthibitishia Hasan kwamba angependa kufanya kitu fulani kipya, na hivyo ndivyo ilivyo," alisema Rummenigge akiiambia Sky Sport Germany.

"Tunatakiwa kukubali hilo. Tuna mkataba ambao upo wazi kwa mwaka mmoja na kama atakubaliana na klabu yoyote italipa ada ya kumchukua."

# DORTMUND WATAKA KUMBAKISHA SANCHO

**DORTMUND, Ujerumani**

MKURUGENZI wa soka wa Borussia Dortmund, Michael Zorc, amesema klabu hiyo ya Bundesliga ingekuwa na furaha kwa Jadon Sancho kubakia kwa msimu wa 2020-21, wakati Manchester United ikiripotiwa kujaribu kufanya mazungumzo na nyota huyo.

Sancho amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka Dortmund kwenda United na miamba hao wa Ligi Kuu ya England wanakaribia kumnasa nyota huyo wa England baada ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.


Hata hivyo, Dortmund hawako tayari kushusha bei ya Sancho, kwani wanataka pauni milioni 109 ili kumuachia aende pale United.

Zorc amezungumzia uvumi huo kuhusu Sancho akisema: "Jadon ni mchezaji wa daraja la juu na katika umri wake ana kipaji cha uhakika kabisa.

"Nitakuwa na furaha kama ataendelea kuwa na sisi msimu unaokuja. Na hilo ndilo ambalo kila mmoja analifikiria hapa."

Sancho mwenye umri wa miaka 20, aliondoka Manchester City kwenda Dortmund mwaka 2017 na haraka akajiimarisha yeye mwenyewe kwenye kikosi cha kwanza cha Bundesliga.

Amefunga mabao 17 kwenye Bundesliga na kutoa pasi za mwisho 16 katika msimu uliomalizika wa 2019-20.



# XHAKA AMSHUKURU ARTETA

**LONDON, England**

KIUNGO wa Arsenal, Granit Xhaka, amebainisha "alikaribia sana" kuondoka klabuni hapo Januari na amemshukuru Kocha Mkuu, Mikel Arteta, kwa kumpa nafasi ya pili.

Xhaka alionekana kama amefunguliwa mlango wa kuondoka wakati alipopokonywa unahodha Novemba kwa kuwaonyesha hasira mashabiki waliokuwa wakimzomea baada ya kutolewa nje kwenye sare ya 2-2 dhidi ya Crystal Palace.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, pia alitemwa kwenye kikosi katika mechi tano, lakini baadaye alirudi kwenye nafasi yake, akianza mara kwa mara.

Arteta wiki iliyopita alimsifia Xhaka kwa kurudisha imani kwa mashabiki kwa kiwango chake cha kuvutia, lakini nyota huyo wa zamani wa Borussia Monchengladbach emebainisha kwamba alikuwa tayari kuondoka.

"Kila mmoja anajua nini kilichotokea kwa upande wangu na mashabiki - au mashabiki na mimi. Haukuwa muda mzuri kwangu," alisema akiiambia BT Sport.

"Lakini pengine ndio ilikuwa sababu ya mimi kuwa imara, hivyo nilijifunza mengi kutokana na hali ile. Natumaini hata mashabiki wameelewa.

"Mara zote nilikuwa najiambia mwenyewe, lakini kwa mashabiki pia, mimi ni mtu nitakayecheza kwa asilimia 100 ya mechi zote."

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uswisi amemshuku-



# SILVA ANUKIA KUTUA LAZIO

**ROME, Italia**

MKURUGENzi wa soka wa Lazio, Igli Tare hajaondoa uwezekano wa kumsajili David Silva kwa uhamisho huru.

Silva ataondoka Manchester City baada ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, akiwa amecheza pale kwa mafanikio kwa kipindi cha miaka 10 katika dimba la Etihad.

Kumekuwa na uvumi kwamba, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, anaweza kujiunga na kikosi cha Lazio kinachonolewa na kocha, Simone Inzaghi, ambacho kimefuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza tangu mwaka 2007-08.

Tare amedai kwamba ni rafiki wa karibu wa kiungo huyo na hivyo hajaondoa uwezekano wa kumchukua.

"Ni mchezaji mkubwa, chochote kinaweza kutokea," alisema Tare akiiambia Sky Sport Italia.

"Nimesikia kutoka kwa marafiki zake kwamba angependa kupata uzoefu mwingine nje ya England, lakini kama nilivyosema mara kwa mara, kuna tofauti kubwa kati ya kusema vitu na kufanya."



# MBAPPE
## NJE DHIDI YA ATALANTA - TUCHEL

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe anahitaji "miujiza" kuwa na nafasi ya kuichezea Paris Saint-Germain kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Atalanta, kwa mujibu wa kocha wake, Thomas Tuchel.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa, aliumia kifundo cha mguu wiki iliyopita kwenye fainali ya Kombe la Coupe de France waliyoshinda dhidi ya Saint-Etienne na ameripotiwa kwamba atakuwa nje ya dimba kwa takribani wiki tatu.

PSG itacheza na Atalanta kwenye mchezo mmoja wa mashindano hayo mjini Lisbon Agosti 12 na Tuchel anaona ni nafasi ndogo sana kwa Mbappe kuwapo kwenye mchezo huo.

"Bado tuna matumaini na kila mmoja anaona kama miujiza kwake kuwapo kwenye mchezo huu," alisema Tuchel akiwaambia waandishi wa habari kabla ya fainali ya Kombe la Coupe de la Ligue ambapo PSG ilikuwa inacheza na Lyon, jana Ijumaa.

"Uwezekano wa kuwapo kwenye kikosi chetu ni mdogo sana, maana inaonekana wazi kabisa kwamba nafasi hiyo ni ngumu kwake.

"Lakini kama kuna miujiza basi inawezekana tukawa naye katika kikosi chetu kwa ajili ya mchezo huu wa robo fainali."

# ANSU FATI KUONGEZA MKATABA BARCA

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA inapanga kumpa mkataba mpya Ansu Fati utakaomuweka hadi mwaka 2024, huku Real Madrid wakimkodolea macho nyota huyo anayetajwa kama "Raphael Varane mpya".

Fati mwenye umri wa miaka 17, amekuwa akihusishwa na mpango wa kuwaniwa Manchester United baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia pale Barca.

Lakini mshambuliaji huyo kinda anaonekana haendi kokote.

Barcelona wanataka kumuongeza mkataba huo Fati baada ya kuonyesha kiwango cha kuvutia kwa kikosi hicho.

Fati ambaye mkataba wake wa sasa unamalizika mwaka 2022, amefunga mabao nane katika mechi 32 msimu huu, akihusishwa zaidi na kuwaniwa na Manchester United.

Gazeti la Sport pia limeripoti kwamba, Barcelona wapo tayari kusikiliza ofa ya mshambuliaji wake, Ousmane Dembele.



## HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARSENAL, CHELSEA NI VITA VYA LONDON LEO

●●●Ni wakati zikikutana katika fainali ya Kombe la FA, rekodi hizi kuamua?...

**LONDON, England**

FAINALI ya Kombe la FA inapigwa leo kwenye dimba la Wembley ikizikutanisha Arsenal na Chelsea.

Klabu hizo pinzani kutoka jiji moja la London, zilikuwa na tofauti kubwa kwenye Ligi Kuu ya England iliyofikia tamati wiki iliyopita.

Kikosi cha kocha, Frank Lampard, Chelsea, kilimaliza nafasi ya nne kweye msimamo wa Ligi Kuu na kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao, huku 'Washikabunduki' wakipitwa pointi 10 wakiwa nafasi ya nane.

Kikosi cha Arsenal cha kocha, Mikel Arteta kinaweza kulitwaa kombe hilo na kufuzu nafasi ya kucheza Ligi ya Europa msimu ujao.

Lakini takwimu hizi hapa chini zinaweza kufifisha matumaini ya Arsenal mbele ya Blues.

**USICHOKIJUA**

Katika mashindano yote, Chelsea imepoteza mechi mbili tu kati ya 10 dhidi ya Arsenal, ikishinda mara tatu na kutoka sare mara tano.

Kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu, Blues waliwafunga Washikabunduki hao mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Emirates kabla ya kutoka sare ya 2-2 pale Stamford Bridge.

Chelsea inacheza fainali yake ya 14 kwenye FA na hii ni mara ya saba kuchezea kwenye Uwanja wa Wembley tangu ulipofunguliwa upya mwaka 2007.

Chelsea imeshinda mara saba kati ya fainali tisa za FA, na zote mbili ilizopoteza ilikuwa dhidi ya Arsenal.

Hii ni mara ya tatu kwa klabu za jiji moja la London kukutana kwenye fainali ya FA, huku Washikabundi hao fainali zilizopita wakishinda mwaka 2002 na 2017 dhidi ya Chelsea.

Arteta alishinda Kombe la FA wakati akiwa anaichezea Arsenal mwaka 2014 na Lampard amecheza fainali tano na Blues hao akishinda mara nne.

Hii ni mara ya tatu kwa misimu minne iliyopita Arsenal kumaliza msimu kwa kucheza dhidi ya Chelsea, ikishinda fainali ya FA ya mwaka 2017 na ikifungwa kwenye fainali ya Ligi ya Europa na Blues hao mjini Baku msimu uliopita.

Straika wa Arsenal, Pierre-Emerick Aubameyang amefunga mabao matatu katika mechi mbili tu za FA.

Raia huyo wa Gabon mabao yote hayo alifunga msimu huu kwenye nusu fainali dhidi ya Manchester City.

## KWA UFUPI

**SANCHO AKARIBIA UNITED**

USAJILI unaokisiwa wa Jadon Sancho kwenda Manchester United uko karibuni kufikiwa, wakati Borussia Dortmund wakiwa tayari kukubali ada ya awali ya pauni milioni 60 kwa ajili ya winga huyo mwenye umri wa miaka, 20. ***(Independent)***

**CHELSEA WAMTAKA STEGEN**

CHELSEA imeweka mezani ofa kwa ajili ya mlinda mlango wa Barcelona, Marc-Andre ter Stegen mwenye umri wa miaka 28. ***(Cadena Ser, via Mail)***

**BALE HAONDOKI MADRID**

GARETH Bale mwenye umri wa miaka 31, amemwambia kocha wa Wales, Ryan Giggs kuwa ana dhamira ya kusalia Real Madrid msimu ujuo, hata kama kukosa michezo kutaathiri kipato chake. ***(Mirror)***

**ALABA LULU CHELSEA, CITY**

CHELSEA na Manchester City ni miongoni mwa klabu zinazoongoza kufuatilia kama mchezaji David Alaba mwenye umri wa miaka 28, atasaini mkataba mpya na Bayern Munich. ***(Telegraph)***

**LIVERPOOL KUMSAJILI KELLY**

LIVERPOOL wanajiandaa kumsajili mchezaji wa Bournemouth, Lloyd Kelly mwenye miaka 21, baada ya kupoteza fursa hiyo miezi 12 iliyopita alipokuwa akiichezea timu ya Bristol City. ***(Express)***

**JIMENEZ HUYO MAN UTD**

MSHAMBULIAJI wa Mexico, Raul Jimenez mwenye umri wa miaka 29, yuko njiani kuelekea Manchester United baada ya Wolves kukubali ada ya pauni milioni 27 kumsajili mshambuliaji wa Braga, Mreno Paulinho. ***(RTP,Express)***

**INTER YAMKOMALIA SANCHEZ**

KLABU ya Inter Milan inatarajiwa kukubali dili kumsajili mshambuliaji, Alexis Sanchez mwenye umri wa miaka 31 kutoka Manchester United kwa mkataba wa kudumu msimu huu. ***(Manchester Evening News)***

**PIERRE-EMILE AKARIBIA SPURS**

KLABU ya Southampton bado wanaisubiri Tottenham kuhusu uhamisho wa kiungo wa kati, Pierre-Emile Hojbjerg mwenye miaka 24. ***(Daily Echo)***

**KLOPP AMUWANIA BREWSTER**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp pia atafanya maamuzi kuhusu mshambuliaji wa Kiingereza Rhian Brewster mwenye umri wa miaka 20, baada ya mchakato wa kucheza kwa mkopo Swansea kufanikiwa. ***(Liverpool Echo)***

**LEEDS YAMUWANIA FABIAN**

KLABU ya Leeds wanapanga kusajili wachezaji wawili- Kiungo wa Everton, Fabian Delph mwenye umri wa miaka 30, na beki Danny Rose mwenye miaka 30, wakati huu ambao kocha Marcelo Bielsa akitafuta wachezaji wenye uzoefu na Ligi Kuu England. ***(Star)***

**ROMERO ANUKIWA TRAFFORD**

GOLIKIPA, Sergio Romero mwenye umri wa miaka 33, anataka kufanya mazungumzo na Manchester United kuhusu mustakabali wake- huku Dean Hanserson mwenye miaka 23, akirejea Old Trafford baada ya kukipiga kwa mkopo Sheffield



HABARI MICHEZO

# HATMA MBAO, MBEYA CITY LIGI KUU BARA LEO

Na Adam Fungamwango

TIMU za Mbao FC na Mbeya City, leo zinatarajia kujua hatma yao ya kubaki kwenye Ligi Kuu au kushuka daraja, zitakapocheza mechi za marejeano za mchujo kwenye viwanja vyao vya nyumbani.

Mbao FC itakuwa kwenye uwanja wao wa nyumbani, CCM Kirumba mjini Mwanza kuikaribisha Ihefu FC katika mechi ambayo itakuwa inaangaliwa zaidi na mashabiki wengi wa soka nchini.

Kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya, Mbeya City itakuwa mwenyeji wa Geita Gold kutoka mkoani Mwanza.

Jumatano iliyopita kwenye mechi za awali, Mbao FC ilikiona cha moto, ilipochapwa mabao 2-0 dhidi ya Ihefu FC kwenye Uwanja wa Highland Estate, Mbalizi, Mbarali mkoani Mbeya.

Kwa matokeo hayo, Mbao ina kazi kubwa ya kufanya, kupata ushindi wa kuanzia mabao 3-0 ili kuwa na uhakika wa kuendelea kubaki Ligi Kuu, vinginevyo msimu ujao itacheza Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara.

"Wao walishinda kwao na sisi tunawakaribisha kwetu Mwanza, haitokuwa mechi rahisi kwao, tutawapa wakati mgumu sana," alisema Waziri Junior, kinara wa mabao wa timu hiyo akiwa amemaliza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa kucheka na nyavu mara 13.

Kocha Mkuu wa Ihefu, Maka Malwisi alisema amejiandaa kikamilifu na mechi ya marudiano na anajua itakuwa ngumu, lakini amewaandaa vijana wake kukabiliana na kila hali.

"Nimeshawandaa vijana wangu kucheza mechi zote mbili, kwa hiyo najua ni jinsi gani na mfumo gani tutacheza," alisema kocha huyo.

Timu ya Mbeya City yenyewe italazimika kupata ushindi wa aina yoyote ile ili kubaki Ligi Kuu kwani katika mechi ya mwanzo Jumatano iliyopita, ililazimishwa sare ya bao 1-1 ikiwa ugenini kwenye Uwanja wa Sekondari ya Nyankungu mjini Geita.

Ihefu FC ilishika nafasi ya pili kwenye Kundi A, huku Geita nayo ikimaliza katika nafasi kama hiyo kwa upande wa Kundi B, wakati Mbeya City, ikishika nafasi ya 15 na Mbao FC ya 16 kwenye Ligi Kuu Bara, hivyo timu zitakazopata matokeo ya jumla zitaungana na zingine 16 kushiriki Ligi Kuu msimu ujao.




Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' (kulia), akimtambulisha kiungo Awesu Awesu juzi, baada ya kumsajili kama mchezaji huru kutokana na kumaliza mkataba na Kagera Sugar. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Azam FC, Abalora waachana, Awesu alamba miaka miwili

Na Saada Akida

UONGOZI wa Azam FC umesema wameachana rasmi na kipa wao namba moja, Razak Abalora na sasa wapo katika mazungumzo na mlinda mlango kutoka ndani ya nchini.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mtendaji Mkuu wa timu hiyo, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema wameachana na kipa huyo baada ya mkataba wake kufika tamati.

Alisema Abarola hawatamuongezea mkataba na wapo katika mchakato wa kuzungumza na kipa kutoka ndani ya nchi atayeongeza nguvu katika kikosi cha timu hiyo.

"Tumeanza usajili kwa kumnasa kiungo kutoka Kagera Sugar, Awesu Awesu kwa mkataba wa miaka miwili kuanzia sasa ni mchezaji halali, tumemsajili kwa kufuata mapendekezo ya kocha wetu, Aristica Cioaba.

Awesu ni miongoni mwa majina 12 ambayo yaliingia katika mchujo hadi kufikia matano na hatimaye kuvutiwa na kiwango cha nyota huyo," alisema Popat.

Alisema mbali na huyo pia muda wowote kuanzia sasa wataendelea kusainisha mikataba wachezaji wao wapya walioafikiana, baada ya kocha kuhitaji kujenga kikosi kipana.

"Kocha anahitaji kuwa na kikosi kipana, hivyo ametaka tusajili winga wa kulia na kushoto, mabeki wote wawili na mshambuliaji mzuri, msimu huu safu ya ushambuliaji haikuwa bora," alisema Popat.

Wakati huo huo, kiungo mpya wa Azam, Awesu ameahidi kufanya makubwa na yenye mafanikio kushirikiana na wachezaji wenzake ndani ya timu hiyo kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema aliwahi kucheza Azam katika kikosi cha vijana kabla ya kuondoka na sasa amefurahi kurejea katika timu yake hiyo kuifanyia makubwa.

"Hakuna mchezaji ambaye hapendi kuja kucheza ndani ya Azam, ni klabu kubwa, nimerejea kufanya kazi ambayo niliianza, nina imani nitazidi kupambana ili kuwa bora zaidi," alisema Awesu.

Kiungo huyo juzi amesaini mkataba wa miaka miwili kuitumikia Azam FC akiwa ni mchezaji huru baada ya dili lake na Kagera Sugar kufika tamati.

## Coastal yazifunda timu Ligi Kuu Bara

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Coastal Union imezishtua timu za Ligi Kuu kutoka kwenye usingizi mzito kwa kuziambia kuwa ziache kushindana mwisho na badala yake zianze kupambana tangu mwanzo ili kutokuwa na wakati mgumu ligi ikielekea ukingoni.

Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Juma Mgunda, alisema hayo akieleza tathmini ya timu yake ya Coastal Union, timu zingine pamoja na Ligi Kuu msimu huu iliyomalizika hivi majuzi.

Alisema ukiondoa tatizo la kidunia la ugonjwa wa COVID-19 unaosababishwa na virusi vya corona, kuna mengi ya kujifunza msimu huu wa ligi.

"Tumejifunza kuwa tukianza kushindana basi anza mwanzo, usisubiri mwisho, unaona sisi tulianza kupambana mwanzo hatukupata matatizo mwishoni mwa ligi, lakini angalia timu zilizokuwa zikiona kama ligi bado, zilivyopata shida mwishoni," alisema Mgunda.

Alisema kwa sasa timu zote zinatakiwa kupambana mwanzo hadi mwisho na si kusubiri mwisho wa ligi, kwani matokeo yake timu nyingi zinafanana pointi, lakini hapo hapo zingine zinabaki na zingine zinashuka.

Kuhusu timu yake alisema kuwa msimu huu ulikuwa mzuri kwake na timu yake kwa ujumla, kwani vijana wake walionekana wamekomaa tofauti na msimu uliopita.

## Simba Queens na siri ya mafanikio

Na Saada Akida

MRATIBU wa Simba Queens, Seleman Erassy, amesema nidhamu na umoja kwa wachezaji wao ni sababu kubwa inayowafanya msimu huu kufanya vizuri na kukaa kileleni mwa msimamo Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Erassy alisema baada ya kutofanya vizuri misimu miwili iliyopita, waliona upungufu wao na kuufanyia kazi mapema ikiwamo nidhamu na umoja wa wachezaji uwanjani.

"Ni kweli kwa wachezaji wa kike bila kuwa mkali lazima wakusumbue, lakini kikubwa tumeliweza kwa sababu moja kubwa yale yote tuliyokubaliana katika mkataba, yote yanatimizwa kwa wakati, kwa hiyo na wao ni lazima wafuate misingi na kanuni za klabu ya Simba, kwa kuhakikisha wanapambana kufika malengo yetu ya kutwaa ubigwa," alisema Erassy.

Alisema wakati wanaanza msimu lengo la kwanza ilikuwa kuhakikisha msimu huu wanakuwa mabingwa wa ligi hiyo ya wanawake ambapo kwa sasa wanaongoza.

"Lengo letu tulipanga tusipoteze mchezo wowote, lakini unavyojua soka hakuna mechi nyepesi, tumepoteza mechi moja dhidi ya JKT Queens, ila sasa hatuhitaji kupoteza tena mechi nyingine," alisema mratibu huyo.

# Michezo

Jumamosi Agosti 1 2020

Nipashe




Arsenal, Chelsea ni vita vya London leo

HABARI UK 22

TUKUTANE KESHO...



Meddie Kagere akisalimiana na umati mkubwa wa mashabiki waliojitokeza kuilaki timu ya Simba, baada ya kuwasili mjini Sumbawanga mkoani Rukwa, juzi, tayari kwa mechi ya fainali ya Kombe la FA dhidi ya Namungo FC itakayopigwa katika Uwanja wa Nelson Mandela kesho. **PICHA: SIMBA**

# TSHISHIMBI AMWAGA MBOGA RASMI YANGA SC

●●● Ashangaa kupewa siku 14 kupitia redioni, amponda Kaimu Katibu Mkuu, asema hajaua kwao hivyo yupo tayari...

**Na Mwandishi Wetu**

SAKATA la usajili wa Kiungo Papy Tshishimbi limezidi kuchukua sura mpya baada ya mchezaji na nahodha huyo wa Yanga kuibuka na kudai kuwa hajaua mtu kwao, hivyo kama klabu hiyo haimtaki yupo tayari kurejea nyumbani ama kutafuta timu nyingine.

Aidha, Tshishimbi 'amemponda' Kaimu Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Wakili Patrick Simon, kwamba licha ya kuwa mwanasheria hajui mambo ya soka kutokana na kwenda kuuzungumzia mkataba wake kupitia redio moja jijini Dar es Salaam.

Awali katika sakata hilo, kiungo huyo alisema bado hajasaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia timu hiyo, na alipoulizwa Simon juzi, alikiri ni kweli na kwamba wamempa siku 14 Mkongomani huyo kufanya uamuzi kuhusu hatima yake ya kusaini ama la.

Simon alisema: "Alifanya mazungumzo na makubaliano yalifikiwa, bado tu kusaini mkataba mpya, baada ya mazungumzo hayo, Hersi Said (GSM) alitueleza viongozi, lakini uongozi wa klabu nao ulitoa mapendekezo yake juu ya kiasi anachokitaka Tshishimbi na tulisema tukipunguze na tumempa siku 14 ambazo zitamalizika Jumatano wiki ijayo," alisema kiongozi huyo.

Lakini baada ya taarifa hiyo, Tshishimbi ameibuka na kumponda kiongozi huyo kwa hatua ya kuuzungumzia mkataba wake redioni huku akishangaa kuambiwa amepewa siku 14 kitu ambacho hajaelezwa.

"Hajui mambo ya mpira (Naibu Katibu Mkuu, Simon Patrick) ingawa ni mwanasheria hawezi kwenda kuzungumzia mkataba wangu redioni, hata hivyo kwetu sijaua mtu, kama hawanitaki naweza kurudi ama kutafuta timu nyingine," alisema Tshishimbi.

Alisema Yanga kama wanataka wao wachukue maana uamuzi ni wao na yeye atatafuta timu nyingine ama kuamua kurejea kwao kabisa.

Kwa mujibu wa Simon, Yanga haina muda wa kuendelea kuvutana na mchezaji mmoja na imemtaka kutoa uamuzi wa kusaini mkataba huo ama, vinginevyo ipo tayari kutazama kwingineko katika kuziba pengo hilo kwa kuwa inaamini wapo wachezaji wengi wazuri wa nafasi hiyo.

"Jukumu lipo kwake ikiwa ataridhika na mkataba tuliompa, atasaini," alisema Wakili Simon huku akieleza Yanga ni taasisi kubwa na hakuna mchezaji au kiongozi ambaye yuko juu ya klabu hiyo, hivyo kazi zote zinafanywa kwa kufuata taratibu.

## SIMBA, NAMUNGO ZAFUNGUKA FAINALI FA

**Na Somoe Ng'itu, RUKWA**

TUKO tayari! Hayo ni maneno kutoka katika benchi la ufundi la Simba ya jijini Dar es Salaam kuelekea mechi ya fainali ya Kombe la FA dhidi ya Namungo FC ya Lindi itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Nelson Mandela Mjini Sumbawanga.

Simba ilitinga fainali ya mashindano hayo baada ya kuwafunga Azam FC katika mechi ya hatua ya robo fainali na baadaye kuwaondoa Yanga kwenye hatua iliyofuata kwa kuwapa kichapo cha mabao 4-1.

Wekundu wa Msimbazi wataingia uwanjani leo huku wakiwa na kumbukumbu ya kushinda Ngao ya Jamii na kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya tatu mfululizo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema wanahitaji kumaliza fainali hiyo 'mapema' ili kukamilisha malengo yao ya kutwaa kikombe cha tatu msimu huu na cha pili chini ya Mbelgiji Sven Vandenbroeck.

Matola alisema wachezaji na benchi la ufundi wako tayari na mchezo huo ambao hautakuwa na presha kubwa kwa sababu tayari timu zote mbili (Simba na Namungo), zimeshakata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa msimu ujao.

"Tulifika Sumbawanga tangu jana (juzi) jioni, na leo (jana) jioni tutafanya mazoezi mepesi ya mwisho, kila mchezaji anajua tunahitaji kurudi na ushindi, ingawa tumewaambia Namungo ni timu nzuri na yenye wachezaji wenye kasi, tunahitaji kuthibitisha ubora wetu wa msimu mzima," alisema Matola.

Naye Kocha Mkuu wa Namungo, Thierry Hitimana, alisema kikosi chake kimejiandaa kukutana na ushindani kwa sababu watacheza dhidi ya timu bora na yenye wachezaji wenye uzoefu wa mechi za michuano mbalimbali.

"Ni mechi kubwa, lakini fainali huwa haina mwenyewe, ukitumia vema nafasi na kujaribu kupunguza makosa, una nafasi nzuri ya kupata ushindi, tunamuomba pia Mungu awe upande wetu, tunahitaji kushinda na kupata kikombe hiki cha kwanza msimu huu," alisema Hitimana.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >